

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)



JAMII FORUMS
WHERE WE DARE TO TALK OPENLY

**TAARIFA YA KAMATI KUFUATIA MATOKEO YA UKAGUZI
MAALUM WA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA
SERIKALI KATIKA AKAUNTI YA TEGETA ESCROW ILIYOKUWA
KATIKA BENKI KUU YA TANZANIA**

OFISI YA BUNGE
S.L.P 941
DODOMA

NOVEMBA 2014

1.0 UTANGULIZI

1.1 Chimbuko la Hoja ya Ukaguzi Maalum wa Akaunti ya Tegeta ESCROW kwa Upande wa Bunge

1.1.1 Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC) kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010

Mheshimiwa Spika, kuwasilishwa kwa Hoja inayohusiana na Akaunti ya Tegeta ESCROW kwa mara ya kwanza ndani ya Bunge lako Tukufu, kulitokana na kuwasilishwa kwa Taarifa ya Mwaka ya iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC) kwa Mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2010.

Mheshimiwa Spika, kuwasilishwa kwa hoja hiyo Bungeni kulitokana na Kamati ya POAC kuchambua na kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwa Mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2009. Mojawapo ya Hoja ya Ukaguzi kwa mwaka husika ilikuwa ni uendeshaji wa Akaunti ya Tegeta

ESCROW ambapo Kamati ilifahamishwa kuwa Kampuni ya IPTL ilikuwa chini ya ufilisi na hivyo kulikuwa na uwezekano wa fedha katika Akaunti hiyo kutolewa na kulipa madeni ya IPTL wakati wa ufilisi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa hiyo, Kamati ya POAC iliwasilisha Bungeni pendekezo la kuzuia utoaji wa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW hadi hapo migogoro yote kati ya TANESCO na IPTL itakapotatuuliwa kwa maslahi mapana ya Taifa na baada ya migogoro hiyo kupatiwa ufumbuzi fedha zilizokuwa kwenye Akaunti hiyo ndio pekee zitumike kulipa madeni ya IPTL.

1.1.2 Kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za

Serikali (PAC) na Gavana wa Benki Kuu Prof. Benno Ndulu

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 Machi, 2014 Kamati ya PAC ilikutana na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha pamoja na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Agizo lililotolewa na iliyokuwa Kamati ya POAC mwaka 2009 kuhusu

matumizi ya fedha zilizokuwemo kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW wakati wa kulipa madeni ya IPTL.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho pamoja na mambo mengine, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania aliiarifu Kamati kuwa fedha zilizokuwemo kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW zimetolewa na kulipwa IPTL. Kamati ilipohoji kama ulipaji huo umezingatia Azimio la Bunge lako Tukufu kwamba fedha hizo zisitolewe mpaka mgogoro baina ya TANESCO na IPTL utakapotatuliwa, haikupatiwa majibu. Hivyo, Kamati kwa kuzingatia umuhimu wa Azimio hilo la Bunge kutekelezwa ipasavyo na kuhakikisha utoaji wa fedha katika Akaunti hiyo umefanyika kihalali na aliyelipwa amelipwa kihalali, ilimuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi Maalum kuhusu miamala iliyofanyika katika Akaunti hiyo pamoja na umiliki wa Kampuni ya IPTL.

1.1.3 **Agizo la Kufanyika kwa Ukaguzi Maalum**

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Machi, 2014 Kamati ya PAC iliwasilisha Hadidu za Rejea kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa

Hesabu za Serikali kwa ajili ya kufanya Ukaguzi Maalum kupitia barua yenye Kumbukumbu Namba CBC.155/188/01/31. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliwasiliana na Katibu wa Bunge kupitia barua Kumbukumbu namba CA.27/442/01/53 ya tarehe 27 Aprili, 2014 ikiomba Kamati ya PAC iweze kuridhia Hadidu za Rejea zitakazoongoza ukaguzi husika. Kamati iliridhia Hadidu za Rejea husika kwa barua Na. CBC. 155/188/01 ya tarehe 3 Mei, 2014.

1.1.4 Majadiliano Bungeni

Mheshimiwa Spika, katika mijadala mbalimbali ambayo imekuwa ikiendelea katika Bunge lako Tukufu, Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wamekuwa wakizungumzia kwa namna tofauti suala la Akaunti ya Tegeta ESCROW. Michango hiyo imekuwa ikijikita katika mambo makubwa mawili, kundi moja limekuwa likidai kuwa fedha hizo ni za umma na zimetolewa bila kufuata taratibu za kisheria. Kundi lingine limekuwa likisema fedha hizo siyo za umma ni za IPTL na zilitolewa kihalali. Baadhi ya Wabunge ambao wamewahi kuzungumzia suala hili ni pamoja na Mhe. David Kafulila, (Mb.) Mhe. John Mnyika, (Mb.), Mhe. Profesa Sospeter Muhongo, (Mb.) Waziri wa Nishati na Madini, Mhe. Stephen

Masele, (Mb.) Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mhe. Jaji. Fredrick Mwita Werema, (*Ex Official*) Mwanasheria Mkuu wa Serikali Waziri Mkuu Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda, (Mb.) Nukuu ya baadhi ya yaliyosemwa na Wabunge hawa zimeainishwa katika uchambuzi wa Kamati ambao ni Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii.

1.2 **Kuwasilishwa kwa Taarifa ya Ukaguzi Maalum**

Mheshimiwa Spika, tarehe 14 Novemba, 2014, Taarifa ya Ukaguzi Maalum wa Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na Miamala iliyofanyika katika Akaunti ya Tegeta ESCROW pamoja na Umiliki wa Kampuni ya IPTL iliwasilishwa kwenye Ofisi ya Spika na Katibu wa Bunge na tarehe 17 Novemba, 2014 ilikabidhiwa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ili ichambuliwe na kutolewa maoni na mapendekezo. Tarehe 18 Novemba, 2014, Kamati ya PAC ilianza uchambuzi wa Taarifa hiyo (**Kiambatisho Na.1**).

1.3 **Kamati ya PAC ilivyofanya kazi**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 119 ya *Kanuni za Bunge, Toleo la 2013* Spika anaweza kukabidhi jambo lingine lolote kwa Kamati yoyote kadri atakavyoona inafaa kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Kamati hiyo. Hivyo, Kamati ya PAC katika kutekeleza jukumu la kuchambua Taarifa ya Ukaguzi Maalum ilifanya kazi kama “Kamati ya Uchunguzi” ikiongozwa na masharti ya *Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296.*¹

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 117 imetoa pia mamlaka kwa Kamati za Kudumu kujiwekea utaratibu wake na kuweza kuwaruhusu Wabunge ambao sio Wajumbe wa Kamati husika kuhudhuria na kushiriki katika shughuli za Kamati. Kwa kutumia Kanuni hiyo, Kamati iliwaalika Mhe. Dkt. Hamisi Kigwangalla (Mb), Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb) na Mhe. Alphaxard Kangi Lugola (Mb) kuhudhuria na kushiriki vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupitia Taarifa ya Ukaguzi Maalum tarehe 19 Novemba, 2014 Kamati ilifanya mahojiano na mashahidi wawili hususan Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ndugu Francis Mwakapalila na Kamishna Mkuu

¹*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, Cap 296*

wa TRA Ndugu Rished Bade. Pia Kamati ilimwandikia Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Dkt. Edward Hosea kama rafiki wa Kamati.

Aidha, Kamati ilipitia Nyaraka na Sheria mbalimbali zilizoletwa na mashahidi pamoja na Kumbukumbu Rasmi (Hansard) za Vikao vya Bunge na Kamati za Kudumu za Bunge ambapo suala la Akaunti ya Tegeta ESCROW limewahi kujadiliwa.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa PAC na Wabunge waalikwa walioshiriki kazi hii ni hawa wafuatao:-

- 
1. Mhe. Zitto Zuberi Kabwe (Mb), - Mwenyekiti
 2. Mhe. Deo Haule Filikunjombe (Mb), - Makamu
Mwenyekiti
 3. Mhe. Asha Mshimba Jecha (Mb), - Mjumbe
 4. Mhe. Desderius John Mipata (Mb), - Mjumbe
 5. Mhe. Zaynab Matitu Vulu (Mb), - Mjumbe
 6. Mhe. Zainab Rashid Kawawa (Mb), - Mjumbe
 7. Mhe. Kheri Ali Khamis (Mb), - Mjumbe
 8. Mhe. Abdul Jabir Marombwa (Mb), - Mjumbe
 9. Mhe. Gaudence Cassian Kayombo(Mb), - Mjumbe

10. Mhe. Hezekiah Ndahani Chibulunje (Mb), - Mjumbe
11. Mhe. Amina M. Mwidau(Mb), - Mjumbe
12. Mhe. Lolesia M. Bukwimba (Mb), - Mjumbe
13. Mhe. Lucy Fidelis Owenya (Mb), - Mjumbe
14. Mhe. Esther Nicholas Matiko (Mb), - Mjumbe
15. Mhe. Ally Keissy Mohamed (Mb), - Mjumbe
16. Mhe. Faida Mohammed Bakar (Mb), - Mjumbe
17. Mhe. Ismail Aden Rage (Mb), - Mjumbe
18. Mhe. Modestus Dickon Kilufi (Mb), - Mjumbe
19. Mhe. Kombo Khamis Kombo, (Mb) - Mjumbe
20. Mhe. Catherine Valentine Magige (Mb), - Mjumbe
21. Mhe. Dkt. Haji Mponda (Mb), - Mjumbe
22. Mhe. Luhaga Joelson Mpina (Mb), - Mjumbe

Mwalikwa

23. Mhe. Alphaxard Kangi Lugola (Mb), - Mjumbe

Mwalikwa

24. Mhe. Dkt. Hamisi A. Kigwangalla (Mb), - Mjumbe

Mwalikwa

Kamati ilisaidiwa na Sekretarieti iliyoongozwa na Katibu wa Bunge

Dkt. Thomas D. Kashililah na Makatibu wengine ambao ni Ndg.

Nenelwa Mwiambi Wankanga, Ndg. Mathew Nionzima Kileo, Ndg.
Mswige Dickson Bisile na Ndg. Erick Sosteness Maseke.



2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI KUHUSU TAARIFA YA UKAGUZI MAALUM NA YALIYOJITOKEZA KWENYE MAHOJIANO YA KAMATI NA KAIMU MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI, KAMISHNA MKUU WA TRA NA MKURUGENZI MKUU WA TAKUKURU

2.1 UTEKELEZAJI WA MKATABA WA TANESCO NA IPTL

Mheshimiwa Spika, katika kuchambua hadidu za rejea zilizofanyiwa kazi na Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati ilijielekeza kwanza kufanya uchambuzi kuhusiana na utekelezaji wa Mkataba wa kuzalisha umeme kati ya Kampuni ya IPTL na TANESCO, uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya Ukaguzi Maalum umebaini mambo mbalimbali. IPTL ilianzishwa chini ya Wanahisa wawili ambao ni Kampuni ya Mechmar Malaysia Berhad iliyosajiliwa nchini Malaysia ambayo ilikuwa inamiliki hisa 7 sawa na asilimia 70 katika IPTL na Kampuni ya VIP Engineering and Marketing iliyosajiliwa hapa nchini ikiwa na hisa 3 sawa na asilimia 30 ya hisa zote. Mwaka 1995 Serikali kupitia TANESCO iliingia Mkataba wa miaka 20 na IPTL kwa ajili ya kuzalisha na

kuuziana umeme wa megawati 100 japokuwa makubaliano ya awali (MOU) yalionyesha kuwa mkataba ungekuwa wa miaka 15. Mahitaji ya umeme ilikuwa ni kwa dharura kutokana na ukame uliosababisha upungufu wa maji katika mabwawa ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1997 ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme ulikamilika. Hata hivyo, TANESCO ilibaini kwamba gharama za ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme ambazo IPTL iliwasilisha kwake zilikuwa kubwa tofauti na makubaliano ya kwenye Mkataba. IPTL ilikuwa imefunga injini zenye msukumo wa kati (*medium speed*) zenye gharama ndogo na uwezo mdogo badala ya injini za msukumo mdogo (*low speed*) zenye nguvu kubwa na bei kubwa. Wakati huo IPTL waliendelea kutoza kiasi kikubwa cha fedha kinacholingana na gharama ya ufungaji wa mtambo wenye msukumo mdogo (*low speed*). Katika utekelezaji wa Mkataba IPTL walitakiwa kufunga jenereta 5 zenye uwezo wa kuzalisha megawati 20 kila moja lakini badala yake walifunga jenereta 10 zenye uwezo wa kuzalisha megawati 10 kila moja jambo ambalo lilikuwa ni kinyume na makubaliano ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, kutokana na IPTL kukiuka makubaliano ya Mkataba kama ilivyoelezwa hapo juu, mwaka 1998 TANESCO ilifungua Shauri Na. ARB/98/8 katika Baraza la Kimataifa la Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji (The International Centre for Settlement of Investment Disputes - ICSID) kupinga ukiukwaji huo. Katika Hukumu iliyotolewa na ICSID, IPTL iliagizwa kupunguza gharama za uwekezaji kutoka USD 163.531 milioni hadi USD 127. 201 milioni kwa mwezi.² **(Kiambatisho Na. 2)**

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mtambo ulikamilika mwaka 1997 lakini uzalishaji na uuzaji wa umeme ulianza mwaka 2002. Kwa mujibu wa makubaliano ya kuzalisha umeme, TANESCO ina wajibu wa kulipia gharama za uwekezaji (*capacity charges*) kwa wastani wa USD 2.6 milioni kila mwezi;³ gharama za kutumia umeme (*energy charges*) wakati uzalishaji halisi unapofanyika na kugharamia mafuta ya kuendeshea mitambo husika. Hivyo, kuanzia mwaka 2002 *capacity charges* ambayo ni gharama za uwekezaji kutokana na uwepo wa mtambo wa kuzalisha umeme,

²Shauri hili hurejewa kama ICSID-1

³ Baada ya utekelezaji wa ICSID 1

zilianza kulipwa na TANESCO kwa IPTL. Ikumbukwe kuwa *capacity charges* huendelea kulipwa kwa muda wote ambao Mkataba unaendelea bila ya kujali kama mtambo unazalisha umeme au hauzalishi.

Mheshimiwa Spika, gharama hizi zilikoma kulipwa moja kwa moja kwa IPTL mwaka 2007 baada ya TANESCO kubaini kuwa IPTL inakokotoa gharama hizo kwa msingi wa USD 38.16 milioni (ambayo ni sehemu ya mkopo wa USD 105 milioni uliochukuliwa na wanahisa kutoka Umoja wa Mabenki ya Malaysia (Consortium of Malaysian Banks) ambao baadaye ulinunuliwa na Standard Chartered Bank ya Hong Kong) badala ya mtaji wa uwekezaji wa kiasi cha Sh. 50,000 uliosajiliwa BRELA na hivyo kufanya tozo ya *capacity charges* kuwa kubwa. Endapo ungetumika mtaji wa uwekezaji wa Sh. 50,000/= katika kukokotoa *capacity charges* TANESCO ingekuwa inalipa tozo ndogo kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutoridhishwa na kiwango cha *capacity charges* kilichokuwa kinatozwa na IPTL mnamo mwaka 2004, TANESCO ilifungua Shauri la Pili ICSID kupinga kiasi kikubwa

cha tozo ya *capacity charges*.⁴ Uamuzi wa Baraza ilikuwa ni kwamba Wanahisa waketi na Mteja wao (TANESCO) na kukubaliana kuhusu kanuni ya ukokotoaji wa tozo hiyo.

Mheshimiwa Spika, mpaka tunapowasilisha Taarifa hii Bungeni, Uamuzi wa ICSID-2 kwamba IPTL ikae na TANESCO kwa ajili ya kukokotoa upya *capacity charges* haujatekelezwa, hivyo TANESCO wanaendelea kulipa USD. 2.6 milioni (sawasawa na shilingi 4,511,000,000/= kwa mwezi)⁵ kila mwezi kama *capacity charges* kwa IPTL izalishe au isizalishe umeme. Hivyo, utekelezaji wa Mkataba wa uzalishaji wa umeme kati ya IPTL na TANESCO umetawaliwa na migogoro toka ulipoanza mpaka sasa.

2.2 UFUNGUAJI WA AKAUNTI YA TEGETA ESCROW

Mheshimiwa Spika, Hadidu Rejea namba tatu ilimtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuchunguza sababu za Kufungua Akaunti Maalumu ya ESCROW – Tegeta (Tegeta-ESCROW Account), Pia kuchunguza Chanzo cha mgogoro kuhusu

⁴ Shauri hili hurejewa pia kama ICSID 2.

⁵ Kiwango cha kubadilishia fedha Dola 1 kwa wastani wa shilingi 1,735 (chanzo BOT tarehe 25/11/2014)

Tozo baina ya TANESCO na IPTL na kuthibitisha iwapo Mgogoro uliamuliwa kwa Masilahi ya pande zote mbili yaani (TANESCO na IPTL).

2.2.1 Chanzo cha kufunguliwa kwa Akaunti ya Tegeta ESCROW

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ukaguzi maalum wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, sababu ya msingi ya kufungua Akaunti ya Tegeta ESCROW ni kipengele Na. 6.8 cha Mkataba wa kununua umeme, (*Power Purchasing Agreement - PPA*) baina ya TANESCO na IPTL ambacho kinaeleza kuwa iwapo upande wowote kati ya TANESCO au IPTL utapinga usahihi wa tozo za Ununuzi wa umeme, Washirika hao watalazimika kutumia jitihada zao kuhakikisha kuwa mgogoro juu ya Malipo husika unamalizika kwa mujibu wa kipengele Na. 18.1 cha PPA.

Mheshimiwa Spika, kipengele husika (18.1 (a)) cha Mkataba wa kununua umeme kinaitaka TANESCO na IPTL kujadiliana iwapo hawaafikiani katika masuala ya Tozo na kinasomeka kama ifuatavyo:

"In the event that a dispute arises, the Parties shall attempt in good faith to settle such Dispute by mutual discussion, which may include referring the Dispute to the Operations Committee, provided that any matters are described in Article 7.4 shall be referred to the Operations Committee for its review and recommendations or attempted resolution, where appropriate"

Mheshimiwa Spika, Aidha, kwa kuzingatia kipengele Na 18.2 (**Kiambatisho Na. 3**) wahusika katika mkataba wa PPA wanalazimika kutumia mtaalamu wa upatanishi (*mediation by expert*) katika utatuzi wa mgogoro kabla ya kutolewa fedha zilizopo kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW.

Mheshimiwa Spika, kipengele cha 18.2 cha mkataba wa ESCROW kinaelekeza wahusika kama ifuatavyo:

"In the event that Parties are unable to resolve a Dispute in accordance with Article 18.1, then

either party, in accordance with this Article 18.2 may refer the Dispute to an expert for consideration of the Dispute and obtain a recommendation from the expert as the resolution to the dispute”

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umethibitisha kuwa kwa muda wote wa Mkataba baina ya TANESCO na IPTL hapakuwahi kuanzishwa Kamati ya Uendeshaji (*Operations Committee*). Kinyume na Kipengele 8.3 (a) cha PPA. TANESCO na IPTL walipaswa kuunda Kamati ya Uendeshaji siku 180 kabla ya kuanza uzalishaji (*Commercial Operation Date*). Kamati hiyo ilitakiwa kuwa na Wajumbe sita ili kuratibu uendeshaji wa mtambo na pia ingehusika na usuluhishi wa migogoro ambayo ingejitokeza kutokana na Mkataba wa uzalishaji umeme.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kufanyika usuluhishi kwenye masuala ambayo TANESCO na IPTL wameshindwa kuelewana umetiliwa nguvu na Kipengele 8.6 cha makubaliano ya Akaunti ya

Tegeta ESCROW. Kipengele hicho kinawaelekeza wahusika kutumia taratibu za usuluhishi na makubaliano kama zilivyoanzishwa na Azimio la Usuluhishi wa Mikataba baina ya Mataifa na Mataifa (ICSID Convention). Hivyo basi ni dhahiri kuwa baada ya TANESCO na IPTL kutokukubaliana katika ngazi ya Kamati ya Uendeshaji (ambayo haikuwahi kuanzishwa) wangekwenda kwa Msuluhishi na kama ingeshindikana wangechukua hatua ya upatanishi (arbitration).

2.2.2 Chanzo cha Mgogoro baina ya TANESCO na IPTL

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, imebainika kuwa chanzo cha mgogoro kati ya TANESCO na IPTL ambacho ndio kilisababisha kufunguliwa kwa Akaunti ya Tegeta ESCROW, ni taarifa ziliyoifikia Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO mnamo tarehe 01 Aprili, 2004. Kaika Taarifa hiyo, pamoja na mambo mengine walifahamishwa na mmoja wa wanahisa wa IPTL, Kampuni ya VIP Engineering, kuwa kuna viashiria kuwa TANESCO wanailipa IPTL *capacity charges* kubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa hiyo, Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO iliiteua Kampuni ya Uwakili ya Mkono ili kufuatilia madai hayo na kutoa ushauri kwa Bodi. Aidha, Bodi iliwateua Ndg. Arnold Kileo, Dr. Enos Bukuku na Bw. Bashiri Mrindoko ambao walikuwa Wajumbe wa Bodi kufuatilia kwa karibu usahihi wa madai hayo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Uwakili ya Mkono iliishauri Bodi ya wakurugenzi ya TANESCO kuwa, gharama za uwekezaji zilizowasilishwa na IPTL na ambazo zilitumika kukokotoa kiwango cha *capacity charges* hazikuwa sahihi. Ushauri huu ulitokana na ukweli kuwa kiwango cha '*capacity charges*' kilichokuwa kinatozwa kilizingatia mtaji wa wanahisa (Owners' Equity) ambao ni USD milioni 38.16 badala ya Sh. za Kitanzania 50,000/= ambazo wanahisa wa IPTL wakati wa usajili wa Kampuni hiyo kwa Msajili wa Makampuni (BRELA) walikionyesha kuwa ndio mtaji (*paid up share capital*). Aidha, kiasi hicho kimeonyeshwa katika Hesabu zilizokaguliwa za IPTL kati ya mwaka 2002 na mwaka 2007.

(Kiambatisho Na. 4).

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ushauri wa Kampuni ya Uwakili ya Mkono, Menejimenti ya TANESCO kupitia barua namba DMDF&CS/02/05, tarehe 17 Juni, 2004 walitoa Notisi kwa IPTL ya kutoendelea kulipa *capacity charges* kwa sababu kiwango walichokuwa wanatozwa ni kikubwa kuliko inavyostahili **(Kiambatisho Na. 5).**

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutoa Notisi hii Kamati imebaini kuwa Bodi na Menejimenti ya TANESCO kwa nyakati tofauti walizitaarifu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Nishati na Madini, na Msajili wa Hazina kuomba zichukue hatua stahiki kutatua mgogoro uliokuwa unaendelea.⁶ Kamati ilifanikiwa kuona barua Na. NEM/740/05 ya tarehe 6 Desemba, 2005 kutoka kwa Kampuni ya Uwakili ya Mkono kwenda kwa aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini Bw. Patrick Rutabanzibwa akirejea mazungumzo yao ya tarehe 5 Desemba, 2005 ambapo iliamuliwa kuwa Kampuni ya Uwakili ya Mkono iandae Rasimu ya Makubaliano kwa ajili ya ufunguzi wa Akaunti ya Tegeta ESCROW.

⁶Barua ya Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali yenye Kumb. Na. SEC/247/07/04 ya tarehe 05 Julai 2004, Barua ya Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO kwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini yenye Kumb. NaSEC.427/9/2004 ya tarehe 23 Septemba, 2004 na Barua ya Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO kwenda kwa Msajili wa Hazina yenye Kumb. Na. SEC.247/8/2004


2.2.3 Kufunguliwa kwa Akaunti ya Tegeta ESCROW

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa Rasimu ya makubaliano ya mchakato wa kufungua Akaunti ya Tegeta ESCROW, Mkataba wa kufunguliwa kwa Akaunti hiyo ulisainiwa na washirika wawili ambao ni Wizara ya Nishati na Madini kama mdhamini wa TANESCO katika ulipaji wa *capacity charges* na *energy charges* na Kampuni ya IPTL. Aidha, kwa mujibu wa Mkataba huo BOT ilikuwa ni wakala wa Uendeshaji wa Akaunti husika.

Mheshimiwa Spika, wakati mahojiano ya Kamati na Kaimu Mdhhibiti na Mbaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamishna Mkuu wa TRA pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU tarehe 19 Novemba, 2014 waliithibitishia Kamati kuwa kutokana na makubaliano wa Akaunti ya Tegeta ESCROW, sehemu ya fedha au fedha yote katika Akaunti hiyo ilikuwa ni fedha ya umma. Katika mahojiano hayo, Maafisa hao walitamka yafuatayo kuhusiana na umiliki wa fedha za Akaunti ya Tegeta ESCROW:

Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

*"... Kwa jinsi tulivyopitia fedha hii, tungenema ipo katika makundi matatu. Kundi la kwanza hiyo fedha ilikuwa na kodi ndani yake kwa hiyo tungenema kulikuwemo na fedha ya Serikali kwa maana ya kodi. Kwa upande mwingine, kwa sababu mpaka ESCROW inafunguliwa kulikuwa na dispute, kulikuwa na kutokubaliana juu ya charges, kwa hiyo kuna fedha ambayo inaweza ikawa ni ya TANESCO na kuna fedha ambayo inaweza kuwa ni ya IPTL ..."*⁷



Kamishna Mkuu wa TRA

⁷Hansard ya mahojiano ya Kamati na Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tarehe 19 Novemba 2014 uk. 19.

*"... TANESCO walitudhihirishia na kwa evidence kwamba katika kufanya yale malipo kwenye ESCROW Account walilipa pamoja na pesa ambayo ilitakiwa kulipwa kwetu ya VAT. Kwa hiyo, kulikuwa na VAT Component ambayo haikutakiwa kwenda kule ..."*⁸

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU

*"... ninachoweza tu kusema na baada ya kusoma Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni wazi kwamba pesa zilivyotoka TANESCO kwenda Benki Kuu bado kwa maoni yetu ni fedha za Serikali kwa sababu ni fedha ya TANESCO. Huo ndiyo mtazamo ambao tunao kiuchunguzi hadi wakati huu."*⁹

Mheshimiwa Spika, majibu haya yaliyotolewa na Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamishna Mkuu wa TRA na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU

⁸Hansard ya mahojiano ya Kamati na Kamishna Mkuu wa TRA tarehe 19 Novemba, 2014 uk. 61.

⁹Hansard ya mahojiano ya Kamati na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU tarehe 19 Septemba, 2014 uk. 81.

yanathibitisha kuwa Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali hawakuwa sahihi walipolieleza Bunge kwamba fedha za kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW siyo za Serikali. Wakijaribu kujibu hoja mbalimbali za Wabunge kuhusiana na suala hilo kwa nyakati tofauti kila mmoja wao kwa namna yake alitamka ifuatavyo:

Waziri wa Nishati na Madini. Mhe. Prof. Sospeter Muhongo (Mb)

“...fedha za ESCROW hizi ni fedha zilizowekwa baada ya hawa wafanyabiashara wawili kutokukubaliana na zingeweza kuwekwa popote ... kwa hiyo hizo pesa ni za IPTL, yaani ni kitu ambacho ni rahisi kabisa, lakini mtu anataka kupotosha hapa anasema fedha za walipa kodi, fedha sijui za wakulima, hakuna kitu kama hicho,”¹⁰

¹⁰Hansard ya tarehe 30 Mei, 2014 ukurasa wa 415

Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mhe. Stephen Masele (Mb)

*"... nilipokuwa namsikiliza Mheshimiwa David Kafulila, nikawa najiuliza maswali, Mheshimiwa David Kafulila yumo humu Bungeni kwa amri ya Mahakama, kama Mahakama inakupa amri ya kuwa Mbunge, halafu leo ikiamua kwamba fedha za IPTL zilipwe, unahoji na unataka umwingize Mheshimwa Muhongo wakati Muhongo hajaamua chochote, kwa kweli inasikitisha."*¹¹

Mwanasheria Mkuu wa Serikali

*"... kuhusu hili la ESCROW, lazima niseme ukweli. Suala la ESCROW ni suala ambalo linatokana na wanahisa wa IPTL ambao ni wanahisa wawili. Mwanahisa mmoja ni VIP na mwingine ni Mechmar, hiyo ndiyo IPTL. Ugomvi huu wa ESCROW siyo pesa ya Serikali (Makofi) ..."*¹²

¹¹Hansard ya tarehe 30 Mei, 2014 ukurasa wa 397

¹²Hansard ya tarehe 25 Juni, 2014 uk. 72.

Mheshimiwa Spika, aidha Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa ni miongoni mwa waliodai kuwa fedha zilizokuwa kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW siyo za umma. Akijibu Mwongozo wa Mheshimiwa Kafulila kwenye Kikao cha Nane, Mkutano wa 15 Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema:

“...fedha zile ambazo zilikuwa zimewekwa ESCROW Account ni fedha za IPTL kwa maana ya hiyo Kampuni. Katika uamuzi wa Mahakama uliotolewa ikaamua kuwa fedha ile ipelekwe IPTL kwa sababu ni fedha ya IPTL. Tukasema ni vyema, kukawa na mvutano pale kidogo sasa tupeleke au tusipeleke, tukasema hapana, uamuzi wa Mahakama unasema pelekeni, fedha zile zikapelekwa kwa sababu ni za IPTL...”¹³

2.2.4 Kuibuka kwa madai ya IPTL Kutaka kulipwa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW

¹³Hansard ya tarehe 9 Aprili, 2014 uk. 50-51

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebainisha kuwa baada ya hukumu ya Mahakama Kuu ya Tanzania katika Shauri Na. 49 la 2002 na Na. 254 la 2003 ya tarehe 05 Septemba, 2013, Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa PAP ambaye sasa anajitambulisha kama Mmiliki wa IPTL, Bw. Harbinder Singh Sethi, alimuandikia Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO barua yenye Kumb. Na. IPTL/TANESCO/2013/03 ya tarehe 13 Septemba, 2013 akimtaka kulipa fedha zote zilizokuwa kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW. (**Kiambatisho Na.6**). barua hiyo ilinakiliwa kwa Waziri wa Nishati na Madini, na hapa ndipo upotoshaji wa amri ya Mahakama ulipoanzia.

Mheshimiwa Spika, Amri ilikuwa inakabidhi '*affairs*' za IPTL lakini haikutoa maelekezo kuwa fedha zilizokuwa kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW zitolewe bila kufuata utaratibu uliokuwa umeainishwa katika makubaliano ya Akaunti husika. Hukumu ya Mheshimiwa Jaji Oriyo ya tarehe 16 Desemba, 2008 iliyokabidhi mali zote za IPTL kwa RITA haikutafsriwa kuwa fedha za Akaunti ya Tegeta ESCROW zitoke bali ziliwekwa chini ya Mfilisi (RITA)

mpaka hapo mgogoro wa *capacity charges* uishe.¹⁴ Ni ajabu kwamba Serikali nzima ilitafsiri Amri ya Mheshimiwa Jaji Utamwa kwa matakwa ya Bw. Harbinder Singh Sethi.

Mheshimiwa Spika, Aidha tarehe 18 Septemba, 2013 Bw. Harbinder Sethi alimwandikia tena Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO akiendelea kuisitiza kuwa TANESCO wakubali kutoa fedha zote za ESCROW na kutoendelea kupinga ankara za madai.¹⁵

Mheshimiwa Spika, kufuatia madai ya PAP kutaka kulipwa fedha zilizokuwa kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW, tarehe 16 Septemba, 2013 Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Bwana Eliakim Maswi, alimwandikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali barua Kumb. Na CBD.88/147/29 akimwarifu kuwa PAP imepewa umiliki wa hisa za IPTL kwa uamuzi wa Mahakama wa tarehe 5 Septemba, 2013. Hata hivyo alimwarifu pia kuwa Akaunti ya Tegeta ESCROW ilifunguliwa kutokana na mgogoro wa *capacity charges* kati hiyo TANESCO na IPTL na hivyo umiliki wa fedha zilizokuwemo kwenye Akaunti ya utabainika baada ya wahusika

¹⁴ Shauri Na. 49 la mwaka 2002, Mahakama Kuu ya Tanzania (Dar Es Salaam)

¹⁵ Barua ya Bw. Harbinder Sethi kwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO yenye Kumb. Na. IPTL/TANESCO/2003 ya tarehe 18 Septemba, 2013

kukutana na kujadiliana juu ya jambo hili. Kaatibu Mkuu aliomba mwongozo wa kisheria kuhusu masuala hayo na akaambatanisha mapendekezo ya makubaliano ya utolewaji wa fedha kwenye Akaunti hiyo yaliyokuwa yameandaliwa na Kampuni ya PAP.

Mheshimiwa Spika, tarehe hiyo hiyo 16 Septemba, 2013 Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Frederick Werema, alimjibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kwa barua Namba AGCC/E.80/6/58 akikubaliana na maoni ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kuwa washirika wa Akaunti ya Tegeta ESCROW (TANESCO na IPTL) wakae pamoja kuchambua madai yanayoihusu TANESCO. Aidha Mwanasheria Mkuu wa Serikali alielekeza kuwa dhamana ya Serikali kwenye Mkataba wa uzalishaji umeme ipitiwe na kujadiliwa upya ili kukidhi mabadiliko yaliyotokea na athari ambazo zingeweza kuipata Serikali.

2.3 MAUZO YA HISA ZA IPTL


Mheshimiwa Spika, Hadidu za rejea Namba 4, 5 na 10 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuchunguza kama wakati

wa kufungua Akaunti ya BOT (Akaunti ya Tegeta ESCROW) Mechmar ilikuwa inamiliki IPTL. Pia, kuthibitisha kwamba kampuni ya Mechmar ilikuwa imehamishia umiliki wake kwa Kampuni ya PAP kabla ya kufilisiwa, na kwamba sasa PAP inamiliki IPTL.

Katika Hadidu Rejea hizi masuala mawili makubwa yamejitokeza, nayo ni mchakato wa PAP kumiliki IPTL na suala la malipo ya kodi ya ongezeko la mtaji (capital gain) na ushuru wa stempu (stamp duty). Kwa upande wa umiliki wa IPTL, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeonyesha kuwa IPTL ilikuwa inamilikiwa na Kampuni mbili, Mechmar (hisa 7) na VIP (hisa 3) kwa mtaji wa Sh. 35,000 kutoka Mechmar na Sh. 15,000 kutoka VIP. Baadaye Mechmar iliua hisa zake 7 kwa Kampuni iliyosajiliwa British Virgin Islands (BVI) iitwayo Piper Link kwa USD milioni 6.

Hata hivyo, uuzaji huu wa hisa kutoka Mechmar kwenda Piper Link ulipingwa katika Mahakama Kuu ya British Virgin Islands kwa Shauri lililofunguliwa na Martha Renju (ambaye anawakilisha masilahi ya Benki ya Standard Chartered Hong Kong). Moja ya maombi yaliyotolewa Mahakamani ni kuwa Mahakama ishikilie Hati

ya hisa husika mpaka shauri la msingi litakapomalizika.¹⁶ Siku hiyo hiyo shauri lilipofunguliwa, tarehe 8 Novemba, 2010 Mahakama ilitoa amri ya kusitisha uuzaji wa hisa hizo saba za Mechmar kwenda Piper Link na kuamuru Piper Link iwasilishe Mahakamani hapo Hati ya hisa 7 za IPTL zinazodaiwa kuuzwa kwake. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imebainisha pia kuwa baada ya uamuzi wa mwisho kutolewa, tarehe 11 Aprili, 2014 Mahakama ilimkabidhi Martha Renju Hati ya hisa saba (7) za Mechmar kwa ¹⁷barua ya Msajili wa Mahakama Kuu ya BVI inayosomeka:



"This is to certify that the Share Certificate No. 01 with 07 shares as defined in the Statement of Claim being held in Custody by The Court in the above matter be returned to Maples and Calder on behalf of the Claimant."¹⁸

¹⁶ BVIH COM 2010/147

¹⁸ Barua ya tarehe 13 Aprili, 2011 kutoka kwa Msajili wa Mahakama Kuu ya BVI kwenda kwa Mawakili wa Martha Rethu – Maples and Calder. Barua hii ni Kielelezo Namba 64 katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Katika mahojiano ya Kamati na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ilithibitishwa kuwa mpaka sasa Hati ya hisa saba (7) za Mechmar kwenye IPTL bado ziko mikononi mwa Benki ya Standard Chartered Hong Kong.¹⁹

Mheshimiwa Spika, umiliki wa hisa unakamilika pale ambapo muuzaji anamkabidhi mnunuzi Hati ya hisa husika, vinginevyo mnunuzi anakuwa amenunua “hisa hewa”. Pamoja na ukweli huu bado Piper Links tarehe 21 Oktoba, 2011 ilimuuzia PAP hisa zile saba kwa gharama ya USD 20 milioni. Swali linalojitokeza hapa ni kuwa unawezaje kuuza kitu usichonacho? Ni wazi kuwa kwa kuwa Piper Links hakuwa mmiliki halali wa hisa saba (7) za Mechmar kwenye Kampuni ya IPTL alichonunua PAP ni “hisa hewa” na kumiliki Kampuni hewa.

Mheshimiwa Spika, Mchakato huo umeifanya Kamati kuhoji uhalali wa PAP kuchukua fedha za ESCROW kwa madai kuwa yeye ndiye Mmiliki mpya wa IPTL. Kutokana na uchambuzi tuliofanya hapo juu kinachojitokeza ni kuwa hata kama kulikuwa na uhalali

¹⁹ Mahojiano ya Kamati na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tarehe 19 Novemba, 2014

kwa IPTL kulipwa sehemu ya fedha zilizokuwa kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW bado PAP hakustahili kulipwa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na mahojiano kati ya Kamati na Kamishina Mkuu wa TRA ilibainika kwamba Kampuni ya Piper Links haijulikani sio tu British Virgin Islands bali hata nchi nyingine.²⁰ Kamati haielewi ni jinsi gani taasisi kubwa kama Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na nyingine zilizohusika katika suala hili, na ambazo tunaamini zimesheheni Watendaji wenye weledi, zimewezaje kushindwa kufanya uchunguzi wa kina (*due diligence*) ambao ungewezesha utata huu kugundulika na kuepuka kudanganywa na PAP.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejiridhisha kuwa kitendo cha Kampuni ya Piper Links kukiuka amri ya Mahakama ya British Virgin Islands ndiyo kilipelekea Bw. Harbinder Singh Sethi kufanya udanganyifu uliotokea. Kwa maana hiyo Piper Links ni chanzo kikubwa cha yaliyotokea. Ikumbukwe kuwa Piper Links na Mechmar walilipa kodi ya ongezeko la mtaji (*capital gain tax*) siku

²⁰ Ndg. Rished Bade, tarehe 19 Novemba, 2014

moja (tarehe 6 Desemba, 2013) na kwenye tawi moja la Benki ya CRDB na wote waliwakilishwa na mtu mmoja aliyewasilisha nyaraka za kughushi na kukwepa kodi ya ongezeko la mtaji iliyopaswa kulipwa.

2.3.1 Kodi iliyopaswa kukusanywa iwapo mauzo ya hisa 7 za Mechmar kwenda Piper Links na baadaye kwenda PAP yangukuwa halali

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kamati umeainisha dosari za kisheria za uhamishaji wa hisa za Mechmar kwenda Piper Links na baadaye Piper Links kwenda PAP. Dosari ambazo zinafanya mchakato huo mzima kukosa uhalali wa kisheria. Hata hivyo endapo mchakato huu ungekuwa halali ulipaswa kuzingatia sheria za kodi hususan Sheria ya Kodi ya Mapato kama ilivyorekebisha na Sheria ya Fedha ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, katika uchambuzi wa Hadidi za Rejea 4, 5 na 10 masuala ya kodi nayo yaliyojitokeza, hususan kodi ya ongezeko la mtaji na ushuru wa stempu. Kaimu Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifafanua kuwa kodi ya ongezeko la mtaji ni kodi ambayo hutozwa

kwenye faida inayotokana na mauzo ya mali na uwekezaji na katika faida itokanayo na mauzo ya hisa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishangazwa na kusikitishwa na kiasi kikubwa cha kodi kilichopotea au kuibiwa kwa makusudi katika mchakato mzima wa ukusanyaji wa kodi husika. Kama ilivyoielezwa hapo awali kuwa, tarehe 9 Septemba, 2012 Kampuni ya Mechmar iliua hisa saba (7) kwa Piper Links ilizokuwa inamiliki katika Kampuni ya IPTL kwa bei ya USD milioni 6.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, taarifa zilizowasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya kukokotoa kiasi cha kodi ya ongezeko la mtaji ambacho Mechmar ilitakiwa kulipa, zinaonyesha kuwa hisa hizo zimeuzwa kwa Sh. milioni 6. Kwa kutumia taarifa hizo, TRA ilikokotoa kodi husika na hivyo Mechmar ilipaswa kulipa kodi ya ongezeko la mtaji Sh. 1,919,988,800 na siyo Tsh.596,500 ilizolipa. Aidha, kwa upande wa ushuru wa stempu Mechmar ilipaswa kulipa shilingi 96 milioni na siyo shilingi elfu 60 ilizolipa. Hivyo jumla ya kodi iliyopotea kwa maana ya kodi ya Ongezeko la Mtaji na ushuru wa stempu ni shilingi 2,015,988,800.

Mheshimiwa Spika, hisa kutoka Piper Links kwenda PAP ziliuzwa kwa gharama ya USD milioni 20, lakini taarifa zilizopelekwa TRA zilionyesha kuwa hisa hizo zimeuzwa kwa USD 300,000. Kwa mantiki hiyo Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonyesha kuwa Piper Links ilitozwa na kulipa kodi ya ongezeko la mtaji kiasi cha Sh. 47,940,000 na Sh. 4,800,000 kama ushuru wa stempu (*stamp duty*). Katika mahojiano, Kamishna Mkuu wa TRA aliifahamisha Kamati kuwa kwa gharama ya USD milioni 20 kiasi cha kodi ya ongezeko la mtaji kilichotakiwa kulipwa ni Sh. 6,399,977,600 na sio Sh. 47,988,800, na kwa upande wa ushuru wa stempu 'stamp duty' kiasi kilichotakiwa kulipwa ni Sh. 320,000,000 na siyo Sh. 4,800,000. Kwa maana hiyo jumla ya kodi iliyopotea kwa maana ya kodi ya ongezeko la mtaji na ushuru wa stempu (*stamp duty*) ni Sh. 6,667,188,800.

Mheshimiwa Spika, jumla ya kodi iliyopotea kutokana na uuzaji wa hisa za Mechmar kwenda Piper Links na za Piper Links kwenda PAP ni jumla ya shilingi 8,683,177,600.

Mheshimiwa Spika, mahojiano ya Kamati na Kamishna Mkuu wa TRA yalilenga, pamoja na mambo mengine, kufahamu jitihada

zilizofanywa na watendaji wa TRA kuthibitisha uhalali wa taarifa zilizowasilishwa kwao (*due diligence*) kabla ya kukokotoa kiasi cha kodi ya ongezeko la mtaji kwa miamala yote miwili yaani Mechmar – Piper Links na Piper Links – PAP. Kamati ilipotaka kufahamu ni hatua gani zimechukuliwa kwa watumishi waliohusika na zoezi hilo, hatua zinazochukuliwa na TRA ili kukusanya kodi iliyopotea na kufuta *Tax Clearance Certificate*, ilijulishwa kuwa kwanza TRA ilishtushwa na taarifa kuwa kulikuwa na mikataba miwili yenye bei tofauti ambayo iliandaliwa na wahusika ili iwawezeshe kukwepa kodi, na kwamba Kampuni ya VIP imeuza hisa zake 3 ilizokuwa ikizimiliki kwenye kampuni ya IPTL kwa bei ya USD milioni 75 wakati PAP hiyo hiyo iliuziwa na Piper Links hisa 7 kwa USD 300,000. Hivyo, TRA ilifanya uchunguzi wake ikiwa ni pamoja na kuhoji watu mbalimbali akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa PAP Bw. Harbinder Singh Sethi (**Kiambatisho Na. 7**).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya uchunguzi wa ndani iliyofanywa na TRA ambao ulithibitisha ukwepaji mkubwa wa kodi na udanganyifu wa mikataba. Kamati imekubaliana na uamuzi wa TRA kuondoa hati za kodi kwa IPTL na hivyo kuna uwezekano kuwa kuanzia tarehe 24 Novemba, 2014 PAP haitokuwa tena

mmiliki wa IPTL mpaka hapo watakapofuata upya tararibu za kisheria na TRA kukusanya kodi stahiki.

2.4 KIASI CHA FEDHA KILICHOKUWEMO NA KILICHOLIPWA KUTOKA AKAUNTI YA TEGETA ESCROW

Mheshimiwa Spika, Hadidu rejea ya 7 ilimtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuchunguza kiwango cha fedha kilichokuwepo kwenye Akaunti Maalumu ya ESCROW, wakati BOT inahamisha fedha zilizokuwepo katika akaunti hiyo kwenda IPTL, kiwango cha cha fedha kilichopaswa kuwemo katika akaunti hiyo maalumu ya BOT pamoja na kiwango cha fedha kinachopaswa kulipwa zaidi kutoka TANESCO. Hii ilihusisha pia kuchunguza na kutoa taarifa kuhusu Kiasi cha fedha kilichowekwa na kila mhusika hadi uamuzi wa mahakama Kuu ya Tanzania ulipotolewa.

Mheshimiwa Spika, hadi kukamilika kwa Ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati imebaini kuwa kiasi kilichokuwepo kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW ni Sh.

167,251,892.330 na USD 22,198,544. Baada ya Uhakiki wa Akaunti ya Tegeta ESCROW hadi tarehe 05 Novemba, 2013 ilikuwa na Kiasi cha Sh. 8,020,522,330 na USD 22,198,544. Aidha, kulikuwa na Kiasi cha Sh. 159,231,370,000 kilichojumuisha fedha zilizowekezwa kwenye hati fungani (Treasury Bills) Sh. 148,071,081,052 zenye riba ya Sh. 11,160,288,948.²¹

Mheshimiwa Spika, malipo yote ya Sh. 167,251,892,330 na USD 22,198,544 zililipwa kwa Kampuni ya PAP kupitia Akaunti Na. 912000012534 ya USD na Akaunti Na. 9120000125294 ya Shilingi za kitanzania katika Benki ya Stanbic zilizofunguliwa tarehe 27 Novemba, 2013 maalum kwa ajili ya kupokea fedha hizo. Hivyo jumla ya fedha iliyotolewa kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW na kulipwa kwa PAP ni shilingi 203,102,540,890.²²

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umebainisha kuwa hadi kufikia tarehe 05 Juni, 2007 kiasi kilichokuwa kwenye akaunti ni jumla ya Sh. 118,291,827,820 japokuwa TANESCO walipinga gharama za tozo, lakini

²¹ Taarifa ya CAG kuhusu Akaunti ya Tegeta ESCROW ukurasa wa 35

²² Kiwango cha kubadilishia fedha Dola 1 kwa wastani wa shilingi 1,615 (chanzo BOT tarehe 28/11/2013)

waliendelea kulipa gharama hizo kati ya mwaka 2004 na 2007. Aidha, uhakiki wa Ankara za IPTL za hadi tarehe 01 Juni, 2014 zilizopatikana TANESCO zilibainisha kuwa Akaunti ya Tegeta ESCROW ilitakiwa kuwa na Sh. 306,675,081,939.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la fedha zilizowekwa katika Akaunti ya Tegeta ESCROW, uhakiki wa wakaguzi ulibainisha kuwa kulikuwa na jumla ya Sh. 182,771,388,687, kati ya hizo TANESCO iliweka Kiasi cha Sh. 142,008,357,587 na Wizara iliweka Kiasi cha Sh. 40,763,031,100.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ankara zilizotolewa na IPTL inaonekana TANESCO ilipaswa kuweka Kiasi cha Sh. 123,903,693,252 zaidi ya fedha ilizoziweka katika Akaunti ya Tegeta ESCROW ikiwa ni tofauti kati ya Kiasi ilichotakiwa kuweka cha Sh. 306,675,081,939 na Kiasi kilichowekwa cha Sh. 182,771,388,687.

Mheshimiwa Spika, pamoja na riba ya Sh. 11,160,288,948 iliyopatikana katika uendeshaji wa Akaunti ya Tegeta ESCROW, fedha hizo zote zililipwa kwa Kampuni ya PAP, huku wakala wa

uendeshaji wa Akaunti husika (BOT) hakupewa kiasi chochote japokuwa walitumia gharama kubwa katika kesi zilizofunguliwa dhidi ya Akaunti hiyo na gharama za kawaida za uendeshaji.

2.5 USHIRIKI WA TAASISI ZA SERIKALI NA WATU BINAFSI KATIKA UTOAJI FEDHA KATIKA AKAUNTI YA TEGETA ESCROW

2.5.1 Benki Kuu ya Tanzania (BOT)

Mheshimiwa Spika, Hadidu ya Rejea ya Pili ilihusu wajibu wa Benki Kuu ya Tanzania kama ulitekelezwa ipasavyo katika mchakato wa kutoa fedha kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW. Miongoni mwa maswali muhimu kwa Kamati ilikuwa ni kwanza kufahamu kwamba katika suala la Akaunti ya Tegeta ESCROW Benki Kuu ilikuwa na Wajibu gani na iliutimizaje? Ama je, ilikuwa sahihi namna Wajibu huo ulivyotimizwa?

Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya Ukaguzi Maalum na Makubaliano ya Uendeshaji wa Akaunti ya Tegeta ESCROW

yaliyokuwepo kati ya Serikali na IPTL umebainisha kwamba Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa na wajibu ufuatao:

a) Kufungua na kuhifadhi Akaunti ya Tegeta ESCROW katika sarafu mbili, yaani Shilingi ya Tanzania na USD.

b) Kupokea, kuhifadhi na kuwekeza fedha za Akaunti ya Tegeta ESCROW;

c) Kushughulikia kutolewa kwa fedha hizo kwa kuzingatia masharti yaliyopo katika Sehemu ya Nne ya Makubaliano ya Akaunti ya Tegeta ESCROW (**Kiambatisho Na. 3**) ambayo ni kujiridhisha kwamba mgogoro kuhusu *capacity charges* kati ya IPTL na TANESCO umetatuliwa, na kwamba Makubaliano yanayohusiana na utatuzi wa mgogoro huo yanakuwepo katika Hati iliyosainiwa na kuwasilishwa kwake kwa ajili ya mchakato wa utoaji wa fedha hizo.

d) Kutoa taarifa za kila robo Mwaka kwa IPTL na TANESCO kuhusu hali ya Akaunti.²³

²³Kipengele Na. 2 cha Makubaliano ya Uendeshaji wa Akaunti ya Tegeta ESCROW

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuchambua namna Benki Kuu ilivyotimiza wajibu wake kama ulivyoelezewa hapo juu tujielekeze kidogo kwenye ufahamu wa dhana nzima ya Akaunti ya Tegeta ESCROW. Akaunti ya aina hii hutumika kuhifadhi kiasi cha fedha pale washirika wa mkataba wa kibiashara wanapokuwa kwenye mgogoro na hivyo kuhitaji kutunza fedha zinazotokana na utekelezaji wa mkataba husika kwenye jambo linalobishaniwa ili kusubiri uamuzi wa msuluhishi au maridhiano ya washirika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyafahamu majukumu ya msingi ya Benki Kuu ya Tanzania katika Akaunti ya Tegeta ESCROW, Kamati ilijielekeza katika kufahamu namna Benki Kuu ya Tanzania ilivyotimiza wajibu huo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba ili kutekeleza wajibu ambao Benki Kuu ya Tanzania ilikuwa nao katika Akaunti ya Tegeta ESCROW, iliishauri Serikali kujiridhisha zaidi kabla ya kutoa fedha kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW juu ya mambo yafuatayo:

- (a) Kuwepo kwa ushahidi kwamba hisa zilizokuwa zinamilikiwa na Mechmar zimenunuliwa na PAP na manunuzi husika yamesajiliwa na BRELA;

(b) Kuwepo na ushahidi kuwa mgogoro uliokuwepo kati ya IPTL na TANESCO kuhusu *capacity charges* umepatiwa suluhu, na imeafikiwa kwamba IPTL ilipwe fedha husika;

(c) Wizara ya fedha ilete ushauri kuhusiana na uwepo wa Kodi ya Ongezeko la thamani katika fedha zilizopo katika Akaunti ya Tegeta ESCROW.

(d) Serikali kupatiwa kinga ya IPTL ili kujiepusha na uwezekano wa kushitakiwa na IPTL hapo baadaye kutokana na Benki Kuu kutoa fedha za IPTL.²⁴

Mheshimiwa Spika, baada ya uchunguzi wa Kamati kuhusiana na ushauri uliotolewa na BOT kwa Serikali yafuatayo yalibainika:

(i) Kuhusu kuwepo ushahidi kwamba hisa zilizokuwa zinamilikiwa na MECHMAR zimenunuliwa na PAP na manunuzi husika yamesajiliwa na BRELA,


²⁴Ushauri wa Benki Kuu ulitolewa kwenye Kikao cha maridhiano kilichoitishwa kwa dharura na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini Bw. Eliakim Maswi kupitia barua yake yenye kumbu Na. CBD. 88/417/31 ya tarehe 23 Septemba, 2013 kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dkt. Servacius Likwelile.

kilichowasilishwa kwa Gavana wa Benki Kuu ni *Deed of Assignment of Shares* na Mkataba wa kuuza hisa kati ya PAP na Piper Link (**Kiambatisho Na. 8**) na siyo hati halisi ya umiliki wa hisa.

(ii) **Kuhusu ushahidi kuwa mgogoro uliokuwepo kati ya IPTL na TANESCO kuhusiana na *overcapacity charges* umepatiwa suluhu na imeafikiwa kwamba IPTL ilipwe fedha husika**, Kamati yangu, imethibitisha kwamba hakukuwa na makubaliano kati ya TANESCO na IPTL ambao ndiyo washirika wa Akaunti ya Tegeta ESCROW. Uthibitisho huu unatokana na maelezo ya kipengele Na. 3.2 na 7.1 cha Taarifa ya Kamati ya Wataalam iliyokutana tarehe 24 Septemba, 2013 kuhusu utoaji wa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW. Taarifa hiyo ya Wataalam ndiyo iliyotumika kama kielelezo cha ushahidi kuwa mgogoro uliokuwepo kati ya IPTL na TANESCO kuhusiana na *capacity charges* umepatiwa suluhu jambo ambalo ni kinyume na yaliyomo katika kipengele 3.2 na 7.1 cha Taarifa husika (**Kiambatisho Na. 9**). Vipengele hivyo vinasomeka kama ifuatavyo:-

"3.2 Discussions between TANESCO and IPTL on disputed capacity charges are ongoing, therefore, the team could not make concrete observation on this issue."

"7.1 TANESCO and IPTL should conclude the ongoing verification of the outstanding capacity charges invoices and issues relating to it and submit a joint resolution to PS-MEM as soon as possible to enable other process to take off."



Mheshimiwa Spika, Kamati imethibitisha kuwa uthibitisho na vielelezo alivyopata Gavana wa Benki Kuu katika kufikia maamuzi ni Taarifa ya Kamati ya Wataalam kama ilivyotajwa hapo juu. Hata hivyo Kamati imefanikiwa kuona nyaraka iliyosainiwa na Ndugu John Kadi kwa niaba ya TANESCO na Mwakilishi wa Kampuni ya IPTL ya tarehe 8 Oktoba, 2013 kwamba wamekubaliana kuwa fedha zote za ESCROW zilipwe kwa IPTL mara moja. Uamuzi huu uliwasilishwa na Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na

Madini tarehe 9 Oktoba, 2013.²⁵ Makubaliano haya hayaonekani katika mawasiliano yoyote ya Kiserikali na badala yake Kamati iliona Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini akiingia makubaliano na IPTL ya utoaji wa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW (**Kiambatisho Na. 10**).

(iii) Kuhusu Wizara ya fedha kupeleka ushauri kuhusiana na uwepo wa Kodi ya Ongezeko la thamani katika fedha zilizopo katika Akaunti ya Tegeta ESCROW, Kamati

haikupata ushahidi kwamba Wizara ya Fedha ilishauri kuhusu masuala ya kodi ya ongezeko la thamani katika fedha zilizokuwepo kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW pamoja na kushauriwa na TRA kwa barua Na. 100-221-969/214 ya tarehe 29 Oktoba, 2013 iliyonakiliwa pia kwa Gavana wa Benki Kuu. Katika barua hiyo TRA waliainisha uwepo wa kodi ya ongezeko la thamani ya Sh. 26,946,487,420.80 kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW (**Kiambatisho Na. 11**). Hata hivyo, barua ya TRA Kumb. Na. TRA/CG/L.3 ya tarehe 4 Februari, 2014 kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha ilionesha kuwa kiasi cha kodi

²⁵barua yenye Kumb. Na. SEC.427/IPTL/10/2013

kinachodaiwa ni Sh. 21,713,935,720.75. (**Kiambatisho Na. 12**).

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa barua yenye Kumb Na. AGCC/E.080/6/70 ya tarehe 18 Novemba, 2013 alimthibitishia Gavana kuwa hakukuwa na kodi ya Serikali katika fedha zilizokuwa kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW na kwamba fedha hizo zihamishiwe IPTL ili Serikali ijinasue na mashauri yasiyo na tija kwake.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ulimptosha Gavana kwa sababu kwa mujibu wa kifungu 5(4) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, 2006 *capacity charges* hukatwa kodi.

(iv) **Kuhusu Serikali kupatiwa kinga kutoka IPTL dhidi ya madai yanayoweza kujitokeza baada ya fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW kulipwa.**

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kinga hii, Harbinder Singh Sethi ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa PAP alitoa Kinga kwa hati iliyotolewa tarehe 27 Oktoba, 2013. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa za TRA zilizowasilishwa kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali uhalali wa PAP kumiliki hisa 7 za Piper Links investment ulitiliwa mashaka na TRA kwa kuwa PAP haikuwa na *Tax Clearance Certificate* ambayo ndiyo hutumika kwa Kampuni kusajiliwa BRELA na hatimaye kutambuliwa na Wizara ya Nishati na Madini. Kwa maana hiyo PAP haikutimiza masharti ya Kifungu cha 90(2) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ambacho kinasomeka kama ifuatavyo:

"The installment referred to in subsection 1 shall be paid before the title to an investment asset is transferred, and appropriate authorities for registration, transfer or approval shall not register such transfer or change of name without the production of a certificate of the Commissioner certifying that the installment has been paid or that no installment is payable."

Mheshimiwa Spika, Kifungu hiki ambacho kilifanyiwa marekebisho kwa Sheria ya Fedha ya mwaka 2012 (Sheria Na 8 ya 2012) kimeweka utaratibu wa kuwezesha Serikali kutoza kodi pale makampuni yanapouziana Hisa nje ya nchi. Sheria hii inataka kwanza kupata hati ya TRA (*Tax Clearance Certificate*) kabla ya BRELA kusajili hisa hizo na kabla ya mamlaka za uthibitisho kuthibitisha. Wakati Wizara inaingia makubaliano ya kutoa fedha za Akauti ya Tegeta ESCROW kwa PAP na wakati PAP wanalipwa fedha hizo, Kampuni hiyo haikuwa na uhalali wa kumiliki IPTL. Hivyo BRELA, Wizara ya Nishati na Madini, TANESCO na BOT walikiuka Sheria ambazo kama zingefuatwa pengine leo tusingekuwa tunajadili suala hili.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana kutoka TRA, imebainika kuwa mpaka malipo ya kwanza katika Akaunti ya Tegeta ESCROW yanafanyika tarehe 28 Novemba, 2013 PAP haikuwa na *Tax Clearance Certificate* ambayo ingeiwezesha kumiliki hisa 7 za IPTL. Taarifa hizo zinaeleza kwamba tarehe 23 Desemba, 2013 kwa kutumia mikataba ya kughushi PAP ilipata Tax Clearance Certificate No. 0049656

(Mechmar kwenda Piper Links) na 0049657 (Piper Links kwenda PAP).

Hata hivyo pamoja na kutokuwa na *Tax Clearance Certificate* bado Kampuni ya PAP ilitambuliwa na Wizara ya Nishati na Madini pamoja na uamuzi wa Mahakama Kuu ya Tanzania wa tarehe 5 Septemba, 2013 kupitia Hukumu ya Mheshimiwa Jaji J.H.K. Utamwa iliyokabidhi shughuli zote za IPTL kwa PAP na kuiwezesha kulipwa fedha zote zilizokuwa katika Akaunti ya Tegeta ESCROW.

Mheshimiwa Spika, Kamati imethibitisha juhudi kubwa aliyofanya Gavana wa Benki Kuu kutaka kujiridhisha vya kutosha kabla ya kuruhusu fedha hizo kutolewa. Hata hivyo, alipata maagizo kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba fedha hizo zitoke **(Kiambatisho Na.17)**.

2.5.2 **Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO**

Mheshimiwa Spika, katika suala la utoaji wa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW, Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO ilikutana katika Kikao cha

dharura mnamo tarehe 19 Septemba, 2013 ili Kujadili suala la utolewaji wa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW. Katika Kikao hicho, Menejimenti ya TANESCO iliwasilisha taarifa Na. 447 ambapo ilitahadharisha juu ya utolewaji wa fedha katika Akaunti hiyo kabla ya kuhitimishwa kwa Shauri la madai ya msingi ya TANESCO juu ya *capacity charges* (**Kiambatisho Na. 13**).

Mheshimiwa Spika, siku hiyo hiyo ya tarehe 16 Septemba, 2013 Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO Jenerali Mstaaafu Robert Mboma, alimwandikia Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini akimwarifu kuwa TANESCO itafuata maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba washirika wa Akaunti ya Tegeta ESCROW wakae pamoja kutatua mgogoro wa *capacity charges* ili kubaini kiasi kinachostahili kulipwa IPTL na kinachotakiwa kurejeshwa TANESCO.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepata shaka kubwa juu ya uamuzi wa haraka bila kufanya uchunguzi wa kina, kwa Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO kufanya vikao viwili mfululizo ili kuruhusu uchochwaji wa fedha za ESCROW. Kikao cha kwanza kilifanyika mnamo tarehe 16 Septemba, 2013 ambapo Bodi ilikuwa

na msimamo sawa na wa Menejimenti kuwa fedha za ESCROW zisitoke, Kikao cha pili cha dharura kikafanyika tarehe 19 Septemba, 2013 ambapo Bodi iliazimia pia kuwa fedha zisitoke.

Mheshimiwa Spika, kati ya tarehe 14 hadi 20 Septemba, 2013 TANESCO ilimuagiza Mwanasheria wake Bw. Godwin Ngwilimi aende nchini Malaysia kufanya “*due diligence*” kuhusu uhalali wa Kampuni ya PAP kumiliki IPTL. Wakati huo Bodi ya TANESCO ilikuwa na vikao vya haraka haraka “supersonic speed” ambavyo vilikubali haraka bila hata kusubiri ushauri wa Mtumishi wao kwamba fedha za ESCROW wapewe PAP.

Mheshimiwa Spika, katika barua ya Mkuu huyo wa Sheria wa TANESCO kwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji yenye Kumbukumbu Na. SEC.427/IPTL/11/2013 ya tarehe 7 Novemba, 2013 alisema:

“Nilishuhudia nyaraka kwamba Piper Link ilinunua hisa za Mechmar na katika mauziano hayo Kampuni hiyo iliwakilishwa na Bw. Harbinder Singh Sethi hivyo huyu bwana ndiye Piper Link na ndiye PAP”

Hata hivyo, Bodi ya TANESCO haikukubaliana na ushauri huo na hatimaye kumwachisha kazi Bwana Godwin Ngwilimi. Kosa lake kubwa ni kutahadharisha kuwa nchi inatapeliwa. Kama ushauri huu ungefuatwa tusingefika hapa tulipo leo kwa sababu hadi hapa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW zilikuwa hazijatolewa.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, mnamo tarehe 9 Oktoba 2013 Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO alimuandikia barua Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini yenye Kumbukumbu Na. SEC.427/IPTL/10/2013 akimuarifu mambo yafuatayo;

- a) Bodi ilipokea kutoka IPTL madai ya kiasi cha ziada cha dola za kimarekani 45,485,719.97 pamoja na riba na tozo ya jumla ya dola za kimarekani 33,564,004.53 na hivyo kufanya jumla ya madai za ziada ya kilichopaswa kulipwa kwenye akaunti ya Tegeta ESCROW kuwa USD 79,049,724.50. Hivyo, kuiagiza Menejimenti ya TANESCO kufanya uhakiki wa kiasi hicho.

- b) Baada ya Menejimenti kuwa imehakiki madai hayo, Bodi imejiridhisha kuwa IPTL sio tu inastahili kulipwa fedha

zilizokuwa kwenye akaunti ya Tegeta ESCROW bali pia wanastahili kulipwa kiasi cha tozo na riba kilichotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, huku ikieleweka kuwa Bodi ya TANESCO haikuwa imefanya maridhiano na IPTL kuhusiana na mgogoro wa 'over capacity charges' unaohusu fedha zilizokuwa kwenye akaunti ya Tegeta ESCROW, Bodi ilimuarifu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini kuhusu makubaliano mapya yaliyofikiwa baina yake na IPTL kuhusu kulipa ziada husika kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW kwa njia mbadala zifuatazo:

- a) Kulipa fedha za ziada dola za kimarekani 45,485,719.97 iwapo TRA itakubali kusamehe kodi ya USD 33,564,004.53 ambayo ni sawa na kiasi cha tozo na riba ambacho TANESCO anadaiwa na IPTL. Au,
- b) Kulipa USD 79,049,724.50 iwapo TRA haitosamehe kodi ya USD 33,564,004.53 ambayo ni sawa na kiasi cha tozo na riba ambacho TANESCO anadaiwa na IPTL (**Kiambatisho Na. 14 na 15**).

Mheshimiwa Spika, Kamati imeshangazwa na makubaliano hayo yaliyofikiwa kati ya Bodi ya TANESCO na IPTL, ikizingatiwa kuwa mgogoro wa msingi uliohusu madai ya TANESCO kutozwa capacity charges kubwa na IPTL haukupatiwa ufumbuzi kama ilivyoelekezwa na ICSID. Kamati imefanikiwa kuona muhtasari wa kikao cha Menejimenti ya TANESCO na IPTL kilichofanyika tarehe 8 Oktoba, 2013 katika Hoteli ya Kunduchi Beach, Dar es Salaam ambapo imebaini kuwa walizungumzia mambo yafuatayo:

a) Hukumu ya Mahakama Kuu ya Tanzania chini ya Mhe. Jaji Utamwa, J iliyotolewa tarehe 5 Septemba 2013

b) Uhamishaji wa mali za IPTL ikijumuishwa Mitambo ya kufua Umeme na madai ya fedha za IPTL kwa TANESCO yaliyowekwa kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW kwenda kwa PAP.

c) Madai ya ziada ya IPTL kwa TANESCO kama yalivyoainishwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, hakukuwa na uthibitisho kuwa walizungumzia suala la kutafuta maridhiano kuhusu madai ya TANESCO kutozwa *capacity charges* kubwa ili kuwezesha kutolewa kwa fedha zilizokuwemo kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW ingawa inaonyesha kwenye mawasiliano mbalimbali yaliyofanyika kati ya Serikali, TANESCO na IPTL walikuwa wanajua kuwa wanapaswa kufanya maridhiano katika suala husika.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kutokana na Bodi ya TANESCO kukubali kulipa madai ya ziada wakati madai ya msingi ya IPTL na TANESCO (Fedha iliyowekwa kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW) hayajapatiwa ufumbuzi, inaonyesha udhaifu wa kiuongozi na kutanguliza maslahi binafsi mbele kabla ya maslahi ya Umma. Kamati inahofu iwapo makubaliano hayo yatakubaliwa na kutekelezwa, Serikali itapoteza fedha nyingi bila manufaa kwa kuendelea kuilipa IPTL madai hayo ya ziada.


2.5.3 **Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya VIP Engineering** **Ndg. James Rugemalira**

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la IPTL, Ndg. James Rugemalira anatajwa kama Mkurugenzi Mtendaji wa VIP Engineering ambaye alikuwa na hisa 3 kati ya hisa 10 kwenye IPTL. Kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, mwaka 2004, Ndg. Rugemalira aliufahamisha uongozi wa TANESCO kuwa gharama za '*capacity charges*' wanazotozwa na IPTL ni za juu tofauti na makubaliano. Taarifa hizi baadaye zilizithibitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO na kusababisha Akaunti ya Tegeta ESCROW kufunguliwa kama tulivyoeleza hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Bw. James Rugemalira ameonekana kuhusika tena na suala la IPTL pale alipofungua Shauri mahakamani kuomba kuiondoa IPTL kwenye ufilisi na kisha kuuza hisa zake kwa Kampuni ya PAP. Ni baada ya uamuzi wa Mahakama Kuu kuhusu shauri hili uliotolewa tarehe 5 Septemba, 2013 ndipo fedha za Akaunti ya Tegeta ESCROW zilipotolewa kwa uharaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia Mkataba wa mauzo ya Hisa kati ya Kampuni ya PAP na VIP na kuthibitisha kuwa Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo (Mb) ndiye

alikuwa kiungo kati ya Bw. Harbinder Singh Sethi wa IPTL na Ndg. Rugemalira wa VIP (**Kiambatisho Na. 16**). Katika mkataba huo wa tarehe 19 Agosti, 2013. Ndg. James Rugemalila alithibitisha kuwa Waziri wa Nishati na Madini Mhe. Prof. Sospeter Muhongo alimwomba kuwasilisha kiasi cha fedha ambacho angependa kulipwa na IPTL ili kumaliza Shauri lililokuwepo mahakamani. Aidha, Bw. Sethi aliwasilisha kwa Bw. Rugemalira ushahidi kwamba PAP imenunua Hisa 7 za Mechmar katika IPTL.



“On 11th July 2013, the Minister of Energy and Minerals, Hon. Dr. Prof. Sospeter Muhongo invited VIP to submit to him the amount of money if paid VIP would conclusively settle VIP claims against IPTL”.

Mheshimiwa Spika, mchakato wote wa kutoa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW ndipo ulipoanza na mauzo ya hisa za VIP kwenda PAP na baadaye kuhitimishwa na maamuzi ya Mahakama Kuu ya tarehe 5 Septemba, 2013 ambayo ndiyo yaliyotumika kuhalalisha utoaji wa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW tarehe 28 Novemba hadi 5 Desemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, Baada ya fedha kutolewa kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW Ndg. Rugemalira alipata mgao wake wa USD million 75, ambazo ndani yake kulikuwa na kodi ya Serikali ambayo haikukusanywa na gharama za uendeshaji wa Akaunti ya ESCROW, fedha hizo zote zilipelekwa katika Benki ya Mkombozi. Huko zilianza kugawiwa kwa watu binafsi. Kamati imearifiwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepeleka suala hilo TAKUKURU na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU amekiri kuendelea na uchunguzi. Kamati pia imekabidhiwa taarifa ya Benki za Stanbic na Mkombozi ambazo zimeonyesha namna ambavyo fedha zilichukuliwa na watu na makampuni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa za benki (bank statements) kutoka Benki ya Stanbic na Benki ya Mkombozi, Kamati ilibaini yafuatayo: -

- a) Kuwepo kwa fedha zilizohamishwa kutoka Akaunti ya PAP iliyoko Benki ya Stanbic kwenda Akaunti ya VIP iliyoko katika Benki ya Mkombozi.

b) Kuwepo kwa fedha taslimu zilizolipwa kwa watu binafsi ambao majina yao hayaonekani lakini walifanya miamala mikubwa kinyume cha Sheria ya Benki Kuu na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006.

c) Kuwepo kwa fedha walizohamishiwa watu mbalimbali katika Akaunti zao binafsi.

d) Katika fedha ambazo zimelipwa kwa watu binafsi katika Benki hizi yapo majina ya viongozi wa kisiasa, viongozi wa madhehebu ya dini, Majaji na watumishi wengine wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inajiuliza ni nini mahusiano ya moja kwa moja kati ya Viongozi hawa na malipo yaliyotokana na Akaunti ya Tegeta ESCROW. Mfano kwa upande wa viongozi wa kisiasa ambao waliingiziwa fedha katika akaunti zao binafsi ni; Mhe. Andrew Chenge (Mb), ambaye alikuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na sasa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, shilingi bilioni 1.6; Mhe. Anna Tibaijuka (Mb) na Waziri wa

Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi shilingi bilioni 1.6; Mhe. William Ngeleja (Mb) na ambaye alikuwa Waziri wa Nishati na Madini shilingi milioni 40.4 na Ndg. Daniel N. Yona ambaye alikuwa pia Waziri wa Nishati na Madini shilingi milioni 40.4; Ndg. Paul Kimiti ambaye ni Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Sumbawanga shilingi milioni 40.4 na Dr. Enos S. Bukuku ambaye alikuwa Mjumbe wa Bodi ya TANESCO aliingiziwa shilingi milioni 161.7.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Majaji Prof. Eudes Ruhangisa, aliingiziwa milioni 404.25 na Mhe. J.A.K Mujulizi aliingiziwa shilingi milioni 40.4.

Mheshimiwa Spika, pia kwa upande wa Watumishi wa umma, Ndg. Philip Saliboko ambaye alikuwa mtumishi wa RITA aliingiziwa shilingi milioni 40.4, Ndg. Emmanuel Daniel Ole Naiko ambaye alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) aliingiziwa shilingi milioni 40.4 na Ndg. Lucy L. Appollo ambaye ni Mtumishi wa TRA aliingiziwa shilingi milioni 80.8.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Viongozi wa Madhehebu ya Dini walioingiziwa fedha na Benki ya Mkombozi ni Askofu

Methodius Kilaini shilingi 80.9, Askofu Eusebius Nzigirwa shilingi milioni 40.4 na Mchungaji Alphonse Twimann Ye Simon shilingi milioni 40.4.

Mheshimwa Spika, Kamati ilithibitishiwa na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU kuwa baadhi ya watu walienda kugawana fedha kwenye Benki tajwa wakiwa na mifuko ya rambo, sandarusi, mabox, magunia na lumbesa. Kutokana na muamala uliofanyika tarehe 6 Februari, 2014 katika Benki ya Mkombozi kiasi cha shilingi bilioni 3.3 na muamala wa Benki ya Stanbic wa tarehe 23 Januari 2014 ambapo fedha taslimu (cash) kiasi cha shilingi bilioni 73.5 zilitolewa na kugawanywa kwa watu mbalimbali kinyume cha Sheria ya Benki Kuu na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006. Taarifa ya benki (bank statements) yenye majina na akaunti zote zilizoingiziwa fedha zimeambatishwa pamoja na taarifa hii **(Kiambatisho Na. 23)**.

2.5.4 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG)

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye mshauri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo ya sheria na anawajibika kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu mambo yote ya kisheria na ushauri wake ni wa mwisho.

Kamati imebaini mawasiliano mbalimbali kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kwa nyakati tofauti wakiomba Ushauri kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusiana na njia bora za kushughulikia suala la Akaunti ya Tegeta ESCROW. Kwa kuzingatia uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na mahojiano, uhusika wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika suala la utoaji wa fedha za ESCROW ni kama ifuatavyo:

a) **Kuruhusu ulipwaji wa fedha za Akaunti ya Tegeta ESCROW kabla ya kujiridhisha na mgogoro uliokuwepo kati ya TANESCO na IPTL**

Mheshimiwa Spika, kufuatia hukumu iliyotolewa na Mheshimiwa Jaji Utamwa mnamo tarehe 05 Septemba, 2013 na baada ya

kupokea barua Na. CAC/184/211/01/23 ya tarehe 30 Septemba, 2013 ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Dr. Servacius Likwelile akiwasilisha taarifa ya Wataalam iliyojumuisha Wataalam kutoka BOT, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Nishati na Madini kuhusu utolewaji wa fedha kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW, Mheshimiwa Jaji Fredrick Werema kupitia barua Kumb. Na. AGCC/E.80/6/65 ya tarehe 02 Oktoba, 2013 alimuarifu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, kuwa ameipitia Ripoti ya wataalamu kuhusu utoaji wa fedha za Akaunti ya Tegeta ESCROW na kwa Maoni yake alisema jambo linaloweza kuleta tatizo katika utoaji wa fedha hizo ni hati fungani zilizowekezwa na Benki Kuu. (**Kiambatisho Na. 17**).

Mheshimiwa Spika, inashangaza kuwa bila ya kufanya uchunguzi wa kina wa mgogoro wa uhamishaji wa hisa za Kampuni ya Mechmar kwenda Piper Links, na kisha kutoka Piper Links kwenda PAP, na ilhali akijua fika kuwa kulikuwa na shauri lililohusu mgogoro wa *capacity charges* kwenye Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi wa migogoro ya Uwekezaji (ICSID 2), Mwanasheria Mkuu badala ya kushauri kupata suluhu ya shauri

lililoamuliwa na ICSID 2 alitumia mamlaka yake kuelekeza fedha za Akaunti ya Tegeta ESCROW kutolewa kwenda IPTL.

Mheshimiwa Spika, ni kwa maelekezo hayo ya mwisho ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Makubaliano ya kutolewa fedha baina ya Wizara ya Nishati na Madini na IPTL yaliafikiwa.

b) **Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya thamani ya Shilingi 23 bilioni.**

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la Mwanasheria Mkuu wa Serikali kusamehe kodi ya Serikali iliyokuwepo katika akaunti ya Tegeta ESCROW, Kamati imebaini kwamba mnamo tarehe 18 Novemba, 2013, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alimwandikia Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania barua yenye Kumb. Na. AGCC/E.080/6/70 akimfahamisha kwamba hapakuwa na kodi ya Serikali iliyopaswa kukusanywa kutoka kwenye Akaunti hiyo. Sehemu ya barua hiyo inaeleza kama ifuatavyo (**Kiambatisho Na. 18**):

“... hata hivyo, katika suala hili la ESCROW Account hakuna kodi inayotakiwa kukusanywa ... kwa sababu fedha iliyopelekwa kwenye kwenye Account haikuwa na VAT iliyolipwa kwa ajili ya capacity charges”

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli huo, Kamati imebaini kwamba maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Gavana wa Benki Kuu, kuwa hapakuwa na kodi ya Serikali iliyopaswa kukusanywa kutoka kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW, yalimsababisha Gavana wa Benki Kuu na hivyo kubariki utoaji wa fedha hizo kabla ya kukata kodi ya Serikali. Aidha maelekezo hayo yalikiuka masharti ya kifungu cha 5(4) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutofanya mawasiliano na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) pamoja na kwamba ana mamlaka ya kutafsiri sheria alipaswa kujiridhisha kwamba hapakuwa na kodi iliyopaswa kukatwa kutoka kwenye fedha zilizokuwa kwenye Akaunti hiyo. Aidha, angeweza kujiridhisha kutoka TANESCO iwapo fedha zilizokuwa zinapelekwa

kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW hazikuwa na kodi ya ongezeko la thamani. Kwa kutotimiza wajibu huo Ofisi yake ilifanya uzembe wa kutokufanya uchunguzi wa kina wa suala hili (*due diligence*) kabla ya kutoa maelekezo kwa Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Gavana yaliikosesha Serikali kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa kiasi cha shilingi 23,154,003,077.

c) **Kutoishauri ipasavyo BOT, Wizara ya Fedha na Wizara ya Nishati na Madini kuhusu kinga kwa Serikali iliyotolewa na PAP**

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 27 Oktoba, 2013, IPTL ilitoa hati ya kinga dhidi ya madai yoyote yanayoweza kujitokeza kwa Serikali na Benki Kuu kuhusiana na fedha zilizokuwa katika Akaunti ya Tegeta ESCROW mara baada ya fedha hizo kulipwa kwa IPTL. Hati hiyo ilisainiwa na Bw. Harbinder Singh Sethi Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa IPTL na kushuhudiwa na Ndg. Joseph Makandege Katibu na Wakili Mkuu wa Kampuni ya IPTL.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyobainishwa katika Ukaguzi Maalumu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ni dhahiri kuwa hisa za Mechmar zilizounuliwa na PAP kutoka Kampuni ya Piper Links ambazo Mahakama Kuu iliziweka chini ya uangalizi wa Martha Renju (Receiver) zina mashaka. Hivyo ilikuwa ni jukumu la Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na mambo mengine kutafsiri vema Hukumu ya Mheshimiwa Jaji Utamwa na kisha kufanya uchunguzi wa kina kujiridhisha juu ya uhalali wa PAP kumiliki hisa za Piper Links zilizohamishwa kutoka Kampuni ya Mechmar.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu tajwa hapo juu ni dhahiri kuwa uhalali wa kinga ya PAP kwa Serikali na BOT kuhusu hatma ya utolewaji wa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW una mashaka, na hivyo kuna uwezekano wa Serikali kushtakiwa na Mechmar muda wowote kwa madai kuwa yenyewe haikuuza hisa zake kwa Piper Links.

2.5.5 **Wizara ya fedha**

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ilikuwa ndio mratibu wa vikao vya Kamati ya Wataalam ya Serikali iliyokuwa ikishughulikia suala la utoaji wa fedha za ESCROW. Uchambuzi wa Kamati umethibitisha kuwa kulikuwa na mawasiliano mbali mbali yaliyokuwa yakifanywa na Katibu Mkuu Wizara ya fedha Ndg. Servacius Likwelile kwenda kwa Gavana wa Benki Kuu na kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kuhusiana na jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha ndiye aliyekuwa kiungo katika kulipatia jawabu suala la utoaji wa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW. Hilo limejidhihirisha pale alipopokea taarifa ya Wataalam na kuiwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na kunakiliwa kwa Gavana wa Benki Kuu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa barua yenye Kumb. Na.CAC/184/211/01/23 ya tarehe 30 Septemba, 2013 kwa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, uhusika wa Wizara ya Fedha hususan Katibu Mkuu Ndg. Servacius Likwelile unaishia katika kuwasilisha taarifa

ya wataalamu ambayo baadaye inafanyiwa kazi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini.

2.5.6 **Bw. Harbinder Singh Sethi**

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa wahusika wakuu wa suala zima la IPTL hususan Akaunti ya Tegeta ESCROW ni Bw. Harbinder Singh Sethi, ambaye anafahamika kama Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa IPTL na wakati huohuo kama Mkurugenzi Mtendaji na Mmiliki wa PAP. Uhusika wake unaanzia katika ununuzi wa hisa saba (7) za Mechmar kwenda Piper Links Investments na kisha kutoka Piper Links Investments kwenda PAP na hatimaye hisa 3 za VIP kwenda PAP na hivyo kumpa umiliki wa IPTL na PAP kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyokwishaafanuliwa hapo awali na
kwa mujibu

wa matokeo ya Ukaguzi Maalumu, ni dhahiri kuwa Bw. Harbinder Singh Sethi hajawahi kuwasilisha hati halisi za uhamisho wa hisa za Mechmar kwenda Piperlinks na kisha PAP. Kwa ushahidi huo ambao unathibitishwa na Maelezo ya Maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kwa nyaraka alizopeleka BRELA kwa usajili wa Kampuni, ni dhahiri kuwa PAP sio Mmiliki halali wa IPTL na wamejipatia fedha za kwenye akaunti ya Tegeta ESCROW kwa njia ya udanganyifu.

2.5.7 MSAJILI WA MAKAMPUNI (BRELA)

Mheshimiwa Spika, uhusika wa BRELA katika suala zima la utoaji wa Fedha

katika Akaunti ya Tegeta ESCROW, unatokana na ushahidi kuwa Kamati imeshindwa kuthibitisha kama Hisa za Piper Links toka Kampuni ya Mechmar na Hisa za PAP toka Piper Links ziliwahi kusajiliwa BRELA kabla Fedha hazijatolewa. Katika uchunguzi wake Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alitilia mashaka mauzo ya hisa hizo baada ya kupata uthibitisho wa uwepo wa hisa 7 za Mechmar kutoka kwa Msimamizi Martha Renju. BRELA ilisajili

umiliki wa hisa za PAP kwa IPTL bila kujali matakwa ya Sheria ya Kodi ya Mapato kama ilivyofafanuliwa hapo awali.

2.5.8 **Wizara ya Nishati na Madini**

Mheshimiwa Spika, Hadidu ya rejea ya tisa ilimtaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuchunguza iwapo Wizara ya Nishati na Madini ambayo iliingia Mkataba na IPTL wa kufungua akaunti Maalumu ya ESCROW ilifanya uadilifu na kuweka uangalifu wa kutosha kabla ya kuingia makubaliano na IPTL ya kutoa fedha zilizokuwepo kwenye Akaunti hiyo na kuilipa IPTL.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini ilikuwa mmoja wa washirika wakati wa ufunguzi na uendeshaji wa Akaunti ya Tegeta ESCROW. Aidha, lilikuwa ni jukumu la Wizara hii kuhakikisha kuwa Maslahi ya Taifa na TANESCO yanalindwa ipasavyo kabla ya kutolewa kwa fedha katika Akaunti husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi maalumu wa

miamala ya Akaunti ya Tegeta ESCROW, Kamati imebaini yafuatayo kuhusu ushiriki na uadilifu wa Wizara ya Nishati na Madini katika suala zima la utoaji wa fedha za ESCROW:

a) Viongozi wa Wizara kutotambua Umiliki wa Fedha za ESCROW

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkataba wa ufunguaji wa Akaunti ya Tegeta ESCROW, washirika wawili katika akaunti hiyo walikuwa ni Wizara ya Nishati na Madini kwa niaba ya TANESCO na IPTL na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ilikuwa ni Wakala wa Akaunti husika kwa ajili ya utunzaji wa fedha na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, uthibitisho wa matamshi ya Viongozi wa Wizara ya Nishati na Madini ya mara kwa mara kuwa umiliki wa fedha za ESCROW ni wa watu binafsi yanatia shaka juu ya uadilifu wao katika kulinda maslahi ya TANESCO na Taifa katika mgogoro uliokuwapo baina ya TANESCO na IPTL.

Kamati imebani kuwa uongozi wa Wizara kwa namna moja au nyingine umefanikisha utoaji wa fedha kwenye akaunti ya

ESCROW Kinyume na kipengele 2.1 cha Mkataba wa ESCROW ambacho kinabainisha kuwa washirika wa Akaunti ya Tegeta ESCROW ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kampuni ya IPTL na sio vinginevyo, kama kinavyonukuliwa hapo chini:

"The ESCROW Agent shall establish and maintain an account, to be held in trust for the benefit of Government of Tanzania and IPTL, and to be designated as the "Tegeta ESCROW Account"

Mheshimiwa Spika, ni kwa msingi huo hapo juu na kwa kuzingatia kuwa Makubaliano ya kufungua Akaunti ya Tegeta ESCROW yalibainisha kuwa wadau wa fedha za kwenye akaunti husika ni Serikali na IPTL, Wizara ya Nishati na Madini haikutimiza wajibu wake ipasavyo ili kuhakikisha haki za TANESCO zinalindwa kabla ya utoaji wa fedha husika hasa kwa dhana iliyokuwa imejengeka miongoni mwao kuwa fedha hizo ni za wanahisa wa IPTL na sio za Serikali au sehemu ya fedha hizo si ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipowahoji Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Kaimu Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Kamishna Mkuu wa TRA walithibitisha kuwa sehemu ya fedha zilizokuwemo kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW ilikuwa ni ya Serikali kwa maana kwamba kwa vyovyote vile palikuwa na fedha za umma katika Akaunti husika.

b) Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini kubadili msimamo wake kuhusu umiliki wa Fedha za kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 16 Septemba, 2013, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini Bw. Eliakim Maswi alimwandikia barua Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na mambo mengine kuomba ushauri wa kisheria kuhusu Akaunti ya Tegeta ESCROW huku akimfahamisha kuwa wamepokea jalada la hukumu ya mahakama kuu kuhusu uamuzi wake wa tarehe 05 Septemba, 2013 uliokuwa ukiiiondoa IPTL kuwa kwenye ufilisi.

Mheshimiwa Spika, katika barua hiyo Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati na Madini anamfahamisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa:

"The ESCROW Account was established as a result of tariff dispute between TANESCO and IPTL on the power generated by IPTL, therefore the ownership of the money in the ESCROW Account will only be established after the tariff dispute is resolved.... We are of the opinion that PAP will be entitled to the amount which belongs to the IPTL after the dispute is resolved and not the entire amount in the ESCROW Account"

Mheshimiwa Spika, pamoja na msimamo huo wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kuwa umiliki wa fedha za ESCROW au sehemu ya fedha hizo ni ya Umma, tarehe 20 Septemba, 2013 siku nne baada ya kuwa na mtizamo kuwa fedha za ESCROW ni za Umma au kiasi chake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini alimjulisha Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa IPTL Bw. Harbinder

Singh Sethi ambaye pia ni Mmiliki wa PAP kupitia barua yenye Kumb. Na. SBD.88/147/01/4 (**Kiambatisho Na. 19**) kuwa Wizara haikuwa na pingamizi dhidi ya kutolewa kwa fedha za ESCROW kama bwana Sethi angewasilisha ushahidi wa kuuzwa kwa hisa asilimia 70 za Mechmar katika IPTL na kutoa kinga kwa Serikali na TANESCO baada ya utoaji wa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imepata mashaka makubwa juu ya sababu iliyomshawishi Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kubadili msimamo na kuondoa masharti yake ya awali kwa Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa IPTL ndani ya siku nne na kuamua kuwa Wizara haioni tena kikwazo cha kuruhusu utoaji wa fedha ikiwa ni Kinyume kabisa na mkataba wa ESCROW uliohitaji kukamilika kwa mgogoro baina ya TANESCO iliyokuwa ikisimamiwa na Wizara na IPTL.

c) Wizara ya Nishati na Madini kutojiridhisha ipasavyo na Uhamishaji wa Hisa za Mechmar kwenda Piper Links na baadaye kwenda PAP

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa uchunguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kisha kuthibitishwa na ushahidi katika mahojiano ya Kamati, imebainika kuwa kuna utata mkubwa kuhusu uhamisho wa hisa za Mechmar kwenda Piperlink na baadaye kwa PAP. Ushahidi uliopatikana hadi Akaunti ya Tegeta ESCROW inafunguliwa ulionyesha kuwa Mechmar ilikuwa mmiliki halali wa IPTL (**Kiambatisho Na. 3**). Aidha, uchunguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulibainisha kuwa Mechmar waliuza hisa zao saba kwa Piper Link Investment mnamo mwaka 2010 kwa USD milioni 6, japokuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alibaini kuwa hati halisi ya umiliki wa hisa hizo bado inashikiliwa na Martha Renju huko BVI, hii inathibitisha kuwa hapakuwa na uhalali wa PAP kumiliki IPTL na kisha kulipwa fedha zilizokuwa kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliendelea kubaini kuwa makubaliano ya uuzwaji wa hisa za Mechmar kwenda kwa Piper Links Investment yamejaa utata mkubwa kutokana na uchunguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kubaini kuwa watia saini katika makubaliano husika hawakuainisha majina yao

dhidi ya sahihi walizoweka, hivyo kutoa tafsiri kuwa kuna jambo lilikuwa linafichwa kwa makusudi. **(Kiambatisho Na. 8).**

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa Wizara ya Nishati na Madini kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara, haikufanya jitihada za kutosha kuhakiki mauziano hayo ya hisa kama alivyokuwa ameomba hapo awali. Katibu Mkuu, Nishati na Madini Ndg. Eliakim Maswi kupokea makubaliano ya uuzaji wa hisa za Piper Links Investment kwenda PAP bila kujiridhisha na kufahamu kuwa hisa hizo zimeshikiliwa na mtu binafsi inathibitisha mashaka ya Kamati kuwa Katibu Mkuu huyo kwa uzembe au kwa makusudi amehusika katika kufanikisha utoaji wa fedha za Akaunti ya Tegeta ESCROW bila kuzingatia taratibu husika.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nishati na Madini ndiyo mamlaka ya kuthibitisha uhamishaji wa umiliki wa Kampuni katika sekta yake. Sheria ya Kodi ya Mapato Kifungu cha 90 (2) kinaitaka mamlaka hii kutotambua uhamisho wa umiliki mpaka kwanza itakapopatikana hati ya kodi kutoka TRA. Kamati iliona Wizara ikiitambua PAP kwa barua zake tu bila kujali matakwa ya kisheria.

d) Wizara ya Nishati na Madini kuingia makubaliano ya utoaji wa fedha za ESCROW bila kupata ufumbuzi wa masuala yenye utata.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapungufu yaliokwishaonekana hapo awali mnamo tarehe 21 Oktoba, 2013 Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini Bw. Eliakim Maswi pamoja na Mwanasheria wa Wizara hiyo Bi. Salome Makange kwa niaba ya Serikali waliingia makubaliano na Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa IPTL, Bw. Harbinder Singh Sethi na Mwanasheria wa IPTL Bw. Joseph Makandegge juu ya utoaji wa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW (Agreement for delivery of funds to Independent Power Tanzania Limited (IPTL) **(Kiambatisho Na. 10)**).

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uchunguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na uchambuzi wa Kamati ambao ulibainisha dosari nyingi zilizotakiwa kufanyiwa kazi na Wizara ya Nishati na Madini kabla ya kusaini makubaliano ya kutoa fedha zilizokuwemo kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW, ni dhahiri kuwa uharaka wa mawasiliano kati ya Wizara ya Nishati na Madini na Kampuni ya PAP hadi kutolewa kwa fedha yanatia mashaka na

ni muhimu kujiuliza uharaka huo ulisababishwa na jambo gani. Suala hili linatia shaka uadilifu wa Viongozi wa Wizara ya Nishati na Madini kwa jinsi walivyoshughulikia.

2.6 MADENI YA IPTL

2.6.1 Uhalali wa Madai ya Benki ya Standard Chartered ya Hong Kong kwa IPTL (USD. 125,970,570.57)

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa madai ya Benki ya Standard Chartered ya Hong Kong kwa IPTL ni halali. Madai hayo yanatokana na Benki hiyo kununua deni la IPTL kwa Umoja wa Mabenki ya Malaysia (*Consortium of Malaysian Banks*) Mwezi Agosti 2005. Kimsingi baada ya TANESCO kuingia Mkataba wa kununua umeme wa IPTL, Kampuni ya IPTL iliingia pia Mkataba na Umoja huo wa mabenki tarehe 28 Juni 1997 kwa ajili ya mkopo wa jumla ya USD. 105,000,000 ili kuwezesha Ujenzi wa mradi wa ufuaji wa umeme uliopo Tegeta. Ingawa, ni kiasi cha USD 85,862,022 tu kati ya USD. 105,000,000 ndicho pekee

kilichopokelewa na IPTL katika ya Mwezi Agosti 1997 hadi Desemba 1999.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kumekuwa na mvutano juu ya uhalali wa madai ya SCB-HK ikielezwa kuwa matakwa ya kifungu Na. 79 (1) na Kifungu Na. 172 vya Sheria ya Makampuni CAP 212 (iliyorekebisha mwaka 2002) hayakutimizwa kwa IPTL kutowasilisha makubaliano yaliyoingwiwa kuhusu deni hili na dhamana zake²⁶, Mdhibiti na Mbaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amethibitisha uhalali wa madai ya SCB-HK kwa kuzingatia yafuatayo:

a) Uamuzi wa Shauri Na. ARB/10/20 lililofunguliwa ICSID ulioeleza kuwa kutosajiliwa kwa makubaliano yenye maslahi ya dhamana 'Security Interest' haiondoi uhalali wa deni dhidi ya Kampuni husika.

b) IPTL ilikuwa ikifanya marejesho hata baada ya deni hilo kununuliwa na SCB-HK, ambapo hadi kufikia mwaka 2007

²⁶ Kifungu cha 79(1) cha Sheria hiyo kinaelekeza kuwa makubaliano yeyote yanayoingwiwa na kampuni iliyosajiliwa Tanzania yanayogusa maslahi katika mali na biashara zake, yanatakiwa yawasilishwe pamoja na nyaraka zinazoshuhudia kwa Msajili wa Makampuni Tanzania ndani ya Siku 42 baada ya tarehe ya makubaliano hayo.

ilikuwa imelipa jumla ya USD 58.69 milioni na kati ya hizo USD 20 milioni zililipwa kwa SCB-HK.

c) Hukumu ya tarehe 5 Septemba, 2013 ya Mahakama Kuu ya Tanzania ilirejesha IPTL kuwa Kampuni hai.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba *capacity charges* humwezesha mwekezaji kulipia mtaji wake (*Return on Equity*) na kulipia mkopo. Kati ya mwaka 2002 hadi 2006 TANESCO ilikuwa inalipa *capacity charges* katika kiwango kamili na hivyo IPTL walipaswa kuwa wamekamilisha kulipa mikopo yao. Aidha, katika kipindi hicho TANESCO ililipa IPTL ziada ya shilingi bilioni 152 ambazo zingepaswa kumaliza deni hilo. Hivyo, deni la USD 125,970,570.57 ambalo Standard Chartered Bank Hong Kong inaidai IPTL linapaswa kulipwa na Mechmar na siyo TANESCO.

2.6.2 Uhalali wa Madai ya TANESCO kwa IPTL (Sh. 321,041,364,000)

Mheshimiwa Spika, Kamati imejiridhisha kuwa madai ya TANESCO kwa IPTL ni ya msingi na yana uhalali ingawa usahihi

wa madai (kiasi cha deni) hayo utapatikana tu baada ya kufanyika kwa mambo yafuatayo;

a) Kutekelezwa kwa uamuzi uliotolewa na Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji cha Kimataifa (ICSID) mwezi Februari 2004 (ICSID 2). Aidha, ICSID 2 ilielekeza TANESCO na IPTL kukokotoa upya kiwango cha *capacity charges*.

b) TANESCO na IPTL kukubaliana kuhusu usahihi wa madai ya TANESCO baada ya washirika hao kukubaliana kuhusu kiwango sahihi cha *Capacity charges*.

2.6.3 Uhalali wa madai ya Watsila Tanzania Ltd (USD. 7,730,018.16) Watsila Netherlands B.V (USD.11,908,195.70 na GBP. 1,439,836.50) kwa IPTL

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Madai ya Watsila Tanzania Ltd USD 7,730,018.16 yanayotokana na utekelezaji wa Mkataba wa uendeshaji na ukarabati wa Mitambo ya IPTL na Madai ya Watsila Netherlands B.V ya USD 11,908,195.70 na Pauni za Kiingereza 1,439,836.50 yanayotokana na utekelezaji wa

Mkataba wa Ujenzi wa Mitambo ya IPTL ni madai halali. Aidha, Kamati imepata uthibitisho kuwa wadeni hao wawili wanaendelea kulipwa na IPTL katika utaratibu waliokubaliana.

2.6.4 Wadai wa IPTL walioainishwa katika Taarifa ya Mfilisi hadi kufikia tarehe 5 Septemba, 2013

Mheshimiwa Spika, kwa sababu zisizoeleweka Taarifa ya Mfilisi wa muda (RITA) iliyotolewa tarehe 5 Septemba, 2013 wakati wa makabidhiano ya IPTL kutoka kwake kwenda kwa PAP, madeni yaliyoorodheshwa yalikuwa ya USD 14,623,062.02 tu bila kujumuisha madai ya Benki ya Standard Chartered ya Hong Kong, TANESCO, Watsila Tanzania Ltd na Watsila Netherlands B.V yaliyoainishwa hapo juu.

2.6.5 Tahadhari iliyochukuliwa na Serikali dhidi ya Madai yanayoweza kujitokeza

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Serikali haikuchukua tahadhari ya kutosha dhidi ya madai mengine yanayoweza kujitokeza kabla ya kutolewa kwa fedha katika Akaunti ya Tegeta

ESCROW. Licha ya kwamba IPTL kupitia barua Na. IPTL/GEN/010-2013 ya tarehe 28 Oktoba, 2013 (**Kiambatisho Na. 20**) iliwasilisha kinga yake kwa Serikali na Benki Kuu dhidi ya madai yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitakiwa kujiridhisha kuhusu uhalali wa PAP kumiliki IPTL na hivyo uhalali wa kinga inayotolewa na IPTL ikizingatiwa kwamba kwa mujibu wa Kamishna Mkuu wa TRA na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU mchakato wa Piper Links kununua hisa za Mechmar na kisha PAP kununua hisa za Piper Links haukuwa halali na TAKUKURU wanaendelea na uchunguzi zaidi kuhusu mauziano ya hisa husika. Kwa sababu hizo, Kamati ina wasiwasi na uhalali wa kinga hiyo suala ambalo linaweza kusababisha hasara kwa Serikali endapo Mechmar itathibitisha kutouza hisa zake kwa kuwa bado zinashikiliwa na mtu binafsi.

2.7 HATUA ZILIZOCHUKULIWA BAADA YA UAMUZI WA MAHAKAMA KUU

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa na jinsi Serikali ilivyotafsiri hukumu ya Mahakama Kuu ya Tanzania chini ya Mhe.

Jaji J.H.K Utamwa iliyotolewa tarehe 5 Septemba 2013 ambayo ikielekeza utekelezaji wa masuala yote matano (5) kama yalivyoombwa na VIP Engineering & Marketing (**Kiambatisho Na. 21**).

Mheshimiwa Spika, Hukumu husika ilihusu utatuzaji wa mgogoro wa wanahisa ambapo, pamoja na mambo mengine ilimuamuru Mfilisi wa muda kukabidhi mali zote za IPTL, ikiwa ni pamoja na mtambo wa kuzalisha umeme kwa Kampuni ya PAP ambayo ilidhamiria kuwalipa wadai wote halali wa IPTL na kuongeza uwezo wa mtambo hadi kufikia MW 500 na kuuza umeme kwa TANESCO kwa bei ya kati ya USD 0.6 hadi 0.8 kwa uniti moja ya umeme.

Mheshimiwa Spika, hukumu hii haikuhalalisha PAP kulipwa fedha zilizokuwa kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW kwa sababu fedha hizo ziliwekwa chini ya makubaliano kati ya Serikali na IPTL kutokana na madai kuwa TANESCO wamekuwa wakitozwa *capacity charges* kubwa. Hivyo, utoaji wa fedha hizo ungefanyika tu kama TANESCO na IPTL wangepata suluhisho la mgogoro huo na kisha kwa pamoja kusaini hati ya makubaliano na kuomba kutolewa kwa fedha hizo wakionyesha kiasi ambacho kinatakiwa

kulipwa kwa mshirika anayestahili kulipwa (**Kiambatisho Na. 3**). Hivyo, kwa Serikali kutumia hukumu hiyo ya Mahakama kama kigezo mahsusi cha kutoa fedha kwenye Akaunti ya Tegeta ESCROW haikuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa pia na jinsi Serikali ilivyojipanga kutekeleza uamuzi huo wa mahakama ikizingatiwa kuwa uamuzi huo unaitaka IPTL kuongeza uzalishaji wa umeme kufikia megawati 500 wakati Mkataba wa kununua umeme (PPA) baina ya TANESCO na IPTL wa mwaka 1995 ulikuwa wa uzalishaji wa megawati 100 tu. Serikali hadi sasa haijapitia na kujadili upya utekelezaji wa Mkataba husika hivyo kuna hatari ya Serikali kupitia TANESCO kuingia katika migogoro mipya.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishangazwa kuona kwamba katika hali isiyo ya kawaida, Mahakama katika Shauri hilo tajwa ilikwenda mbali zaidi hadi kupanga kiwango cha bei ya umeme kuwa USD 0.6 hadi 0.8 kwa uniti moja ya umeme, ikizingatiwa kuwa bei ya umeme hupangwa katika mkataba wa mauziano ya umeme au mwenendo wa soko.

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

3.1 MAONI YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia hadidu rejea kumi zilizochambuliwa hapo juu na kuzipatia majibu yote kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi maalum katika akaunti ya Tegeta ESCROW, Kamati inapaswa kutoa mapendekezo ya njia sahihi za kisheria zinazoweza kutumika kwa ajili ya kulinda Serikali isipate hasara tena katika utekelezaji wa Mkataba wa Uzalishaji umeme kati ya TANESCO na IPTL. Vilevile Kamati inatoa mapendekezo juu ya hatua stahiki ambazo zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya wahusika kulingana na matokeo ya ukaguzi maalumu.

Mheshimiwa Spika, Kamati imethibitisha bila chembe ya mashaka kwamba mchakato mzima wa kutoa fedha katika akaunti ya Tegeta ESCROW uligubikwa na mchezo mchafu na haramu wenye harufu ya kifisadi ulioambatana na udanganyifu wa hali ya juu ambao kwa kufuata sheria tu ungeweza kugundulika na kuzuiwa. Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, mfumo mzima wa Serikali ni kama ulipata ganzi au uliganzishwa ili kuwezesha zaidi ya shilingi bilioni 306 kuporwa kutoka Benki Kuu ya Tanzania na kutakatishwa kupitia Benki mbili hapa Nchini na baadhi ya mabanki ughaibuni.

Mheshimiwa Spika, Kamati imethibitisha kuwa hukumu ya Jaji Utamwa ya kukabidhi masuala yote ya IPTL kwa Kampuni ya PAP, ilitafsiriwa vibaya kwanza na Bwana Harbinder Singh Sethi mwenyewe na baadaye ikatafsiriwa vibaya pia na viongozi wa Wizara ya Nishati na Madini, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hata baadhi ya viongozi wakuu wa Serikali akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tafsiri hii potofu ilirudiwa rudiwa na kuimbwa na viongozi wa Wizara kiasi cha kuliaminisha Bunge na Umma kwamba ndio ilikuwa tafsiri sahihi. Baada ya kupata ushahidi usio na mashaka kutoka kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za

Serikali na Mamlaka ya Mapato Tanzania, ni dhahiri Kampuni ya PAP haikuwa na uhalali wowote wa umiliki wa IPTL wakati inalipwa fedha za kutoka Akaunti ya Tegeta ESCROW.

Mamlaka ya Mapato Tanzania kupitia uchunguzi wake imebaini kukiukwa kwa Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 333, kifungu cha 90 (2) kama ilivyofanyiwa marekebisho na sheria ya Fedha, sheria namba 8 ya mwaka 2012 kuhusiana na mabadiliko ya umiliki wa hisa kutoka Kampuni moja kwenda nyingine zilizoko nje ya Tanzania na zenye mali hapa Tanzania. Vile vile uchunguzi umeonyesha ukwepaji mkubwa wa kodi uliotokana na kuwasilisha nyaraka za kughushi kulikofanywa na mawakala wa Kampuni ya PAP ambapo hata kama wangukuwa wamefuata sheria hiyo hapo juu bado wangukuwa wamesababisha ukwepaji kodi wa shilingi 8.7 bilioni.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 19 mwezi Novemba 2014, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania alimwandikia barua Msajili wa Makampuni (BRELA) akionesha kusudio la kuondoa uhalali wa hati za malipo ya kodi ya ongezeko la mtaji (capital gains tax certificates) zilizolipwa kuthibitisha mauzo ya hisa

za Mechmar kwenda Piperlink na baadaye PAP akitoa siku 6. Barua hii iliwasilishwa mbele ya Kamati. Hivi sasa tunavyowasilisha taarifa hii siku sita zilikamilika jana bila Kampuni ya PAP kuchukua hatua zozote za kufanya malipo halisi na halali kama Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato alivyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, CAG amebainisha pia kuwa Bwana Harbinder Singh Sethi hana hati halisi ya hisa za Kampuni ya Mechmar katika IPTL maana zilizuiwa na Mahakama ya British Virgin Island. Hivyo Kamati inaitaka Serikali kwenda mahakamani kuomba mapitio ya hukumu ya Jaji Utamwa, J na kwa kutumia ushahidi huu ili kuirejesha IPTL katika hali iliyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imeridhika kuwa Mkataba wa IPTL uligubikwa na tuhuma za ufidiaji toka kuanza kwake, tuhuma ambazo mara kadhaa zimethibitishwa na maafisa waandamizi wa Serikali na hata Baraza la Kimataifa la Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji (ICSID 1) kupelekea kushusha gharama za uwekezaji wa mitambo hiyo. Mkataba huu pia umekuwa ukikiukwa mara kwa mara bila kujali (*impunity*) ikiwemo kukosekana kwa Kamati ya pamoja ya uendeshaji kama ilivyoonyeshwa katika taarifa ya CAG.

Kamati inaitaka Serikali, kwa mujibu wa Sheria na kwa kutumia mkataba wa mauziano umeme kati yake na IPTL, kuuchukua mtambo huu na kuumilikisha kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba Benki ya Standard Chartered ilikuwa na madai yake katika IPTL kufuatia kununua deni lililotolewa kwa IPTL na mabanki ya Nchini Malaysia. Vile vile Kamati imethibitisha kuwa mkopo uliotolewa ni wa thamani ya Dola za kimarekani 105 milioni, lakini zilizotumika kwa ajili ya mradi huu ni Dola za kimarekani 85 milioni tu. Hata hivyo, Kamati inapenda kulifahamisha Bunge lako tukufu, kama tulivyokwisha sema huko awali, kwamba kupitia malipo ya *'capacity charges'* kati ya mwaka 2002 – 2006 ambapo TANESCO ililipa ziada ya shilingi 152 bilioni, deni hili lilipaswa kuwa limelipwa.

Ikumbukwe kuwa *'capacity charges'* ni malipo ya mtaji na mkopo na sio malipo ya huduma ya umeme ulionunuliwa. Kwa maana hii Benki ya SCB-HK haipaswi kuwa na madai yeyote yale dhidi ya Serikali ya Tanzania au TANESCO wala haki ya dhamana ya

Serikali kwa IPTL. Kwa kuwa Kamati inapendekeza kuchukuliwa kisheria kwa Kampuni ya IPTL na kuimilikisha kwa Shirika la TANESCO, Serikali ielekezwe kwanza kuchunguza malipo ya '*capacity charges*' yaliyolipwa kati ya mwaka 2002 – 2006 kama yalihudumia mkopo kabla ya makubaliano yeyote na Benki ya SCB – HK ili kukwepa kulipa mkopo huo mara mbili.

Mheshimiwa Spika, Kamati imethibitisha kuwa Bwana Harbinder Singh Sethi kwa makusudi na kwa lengo la kujitwalia fedha alifanya udanganyifu, kuwasilisha nyaraka za kughushi za umiliki wa hisa 70% za Kampuni ya Mechmar katika Kampuni ya IPTL kwenda Kampuni ya PiperLink iliyopo '*offshore*' na kisha kwenda Kampuni anayomiliki ya PAP. Vile vile Bwana huyu alifanya ujanja kwa kushirikiana na viongozi waandamizi wa Serikali, maafisa wa BRELA na maafisa wa ngazi ya chini wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na hivyo kufanikiwa kuchota fedha asizostahili jumla ya shilingi 306 bilioni kutoka Benki Kuu ya Tanzania. Fedha hizo ziliwekwa katika akaunti nambari 9120000125294 ya Kampuni ya PAP iliyopo Benki ya Stanbic, jijini Dar es Salaam, akaunti ambayo ilifunguliwa tarehe 28 Novemba 2013 kwa kazi maalumu na kisha kufungwa tarehe 16 Septemba, 2014. Kamati imeridhika kuwa

Bwana Harbinder Singh Seth alikiuka Sheria za kodi, alijipatia mali asiyostahili na hivyo kuhujumu uchumi wa Nchi yetu na alitakatisha fedha haramu kwa kuzitumia kununua hisa 30% ya Kampuni ya VIP inayomilikiwa na Bwana James Rugemalira kwa thamani ya dola za kimarekani 75 milioni.

3.2 Kamati inapendekeza kama ifuatavyo: -

3.2.1 **Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Kuzuia na kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI) mara moja wachukue hatua ya kumkamata Bwana Harbinder Singh Sethi na kumfikisha mahakamani kwa makosa ya *Anti money laundering*, ukwepaji kodi na wizi. Kamati pia inaelekeza Serikali kutumia sheria za Nchi, ikiwemo sheria ya *'Proceeds of Crime Act'* kuhakikisha kuwa Bwana Harbinder Singh Sethi anarejesha fedha zote alizochota kutoka Benki Kuu ya Tanzania. Kwa kuwa suala hili ni suala la utakatishaji wa fedha haramu, Mamlaka ziwasiliane na mamlaka za Nchi nyingine kuhakikisha mali za Bwana huyu zinakamatwa na kufidia fedha hizo.

3.2.2 **Mheshimiwa Spika**, Kamati imethibitsha kuwa Bwana James

Rugemalira aliuza hisa ambazo Kampuni yake ya VIP inamiliki katika IPTL na kulipwa na Bwana Sethi kutoka katika Fedha za Akaunti ya Tegeta ESCROW. Kamati imethibitisha kuwa fedha kutoka akaunti za Kampuni ya PAP katika Benki ya Stanbic zilizofunguliwa maalumu kwa ajili ya kupokea fedha kutoka Akaunti ya Tegeta ESCROW iliyokuwa Benki Kuu zilipelekwa katika Akaunti nambari 00151002368801 na Akaunti nambari 00151002368802 za Kampuni ya VIP ziliyopo Mkombozi Commercial Bank.

Kwa mujibu wa Taarifa ya CAG na kuthibitishwa na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU fedha hizo pia ziligawiwa kwa watu mbalimbali binafsi. Kamati haina tatizo na watu wawili kuuziana makampuni yao kwa thamani wajuazo wenyewe, au jinsi ya kuzitumia fedha zao, ama kuwachagua watu wa kuwagawia, lakini Kamati imejidhihirishia kuwa fedha iliyotumika kulipia manunuzi hayo ni fedha ambayo sehemu yake ni ya umma iliyochotwa bila huruma wala aibu, kutoka Benki Kuu. Hivyo, Kamati inazitaka mamlaka za uchunguzi kuhakikisha kuwa fedha hizo zinarudi Benki Kuu hata ikibidi kwa kufilisi mali za watu wote

waliofaidika na fedha hizo kwa thamani ya fedha walizopewa na Bwana Rugemalira.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya waliofaidika na fedha hizo ni Viongozi wa Umma ambao wanapaswa kuzingatia Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Sheria namba 13 ya Mwaka 1995) ambayo inawataka kutoa taarifa ya zawadi wanazopokea au malipo wanayolipwa. Vyombo vya uchunguzi vifanye uchunguzi kutambua kama walifuata matakwa ya sheria na hatua mahsusi zichukuliwe, ikiwemo kuvuliwa nyadhifa zao zote za kuchaguliwa na/au kuteuliwa, kufilisiwa mali zao na kushtakiwa mahakamani kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 132 (1) – (6).

3.2.3 **Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imethibitisha kwamba fedha zilizolipwa kwa Watu binafsi zilitokana na Akaunti ya Tegeta ESCROW zilizolipwa kwa PAP ambayo si mmiliki halali wa IPTL. Kwa maana hiyo fedha hizo zilitolewa kwa watu hao kama rushwa na kuzitakatisha fedha hizo haramu. Aidha, kamati inapendekeza kwamba Akaunti zote zilizohusika na miamala hii haramu ya Akaunti ya Tegeta ESCROW, akaunti zao zifungwe (*freeze*) na

wenye akaunti hizo walazimishwe kurejesha fedha hizo kwa mujibu wa Sheria (Anti Money Laundering) ikiwa ni pamoja na mali zao kufilisiwa. Kwa upande wa viongozi wa Kisiasa wawajibike na Watumishi wa umma wafukuzwe kazi.

3.2.4 Mheshimiwa Spika, Kamati imejiridhisha kwamba, suala la akaunti ya Escrow ni jambo la utakatishaji wa fedha (Money Laundering), kama alivyosema Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU katika mahojiano yake na Kamati. Kamati inazitaka mamlaka zinazohusika, ikiwemo Benki Kuu kuzitangaza benki za Stanbic na Mkombozi Commercial Bank kama asasi za utakatishaji fedha (Institutions of Money Laundering Concern).

3.2.5 Mheshimiwa Spika, Aidha, Kamati inalikumbusha Bunge lako tukufu pendekezo muhimu lililotolewa na Kamati Teule ya Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kuhusu sakata la maarufu la Richmond. Kamati ilipendekeza:

"Mkataba kati ya TANESCO NA Richmond Development Company LLC na sasa Dowans Holdings S.A. kama ilivyo mikataba kati ya TANESCO na IPTL, SONGAS, AGGREKO

na Aistom Power Rentals inatoa unafuu usiostahili kwa makampuni hayo ya umeme na kuiumiza TANESCO na hatimaye watumiaji na walipa kodi kimapato, k.m. mikataba hiyo kuwa na vipengele vya kuibana TANESCO kuyalipa makampuni hayo kodi zinazohusika na uendeshaji (operations) matengenezo/marekebisho ya mara kwa mara ya mitambo (maintenance) gharama za bima, ada za mawakili na washauri elekezi (consultants) gharama za mafuta na gesi ya kuendeshea mitambo, gharama za ukodishaji mitambo (capacity charges) ambazo TANESCO hulipa kila mwezi si chini ya wastani wa shilingi bilioni 2 kwa kila kampuni, izalishe au isizalishe umeme. Kamati Teule inatoa rai kwa Serikali kuwa mikataba yote hii ipitiwe upya mapema iwezekanavyo kama ambavo mikataba ya madini knavyopitiwa upya sasa na Serikali. Bila kufanya hivyo, mzigo mkubwa wa gharama za umeme utawaelemea wananchi na kushindwa kufikia azma ya Serikali ya maisha bora kwa kila Mtanzania.”

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, azimio hili litekelezwe kwa kupitia upya mikataba yote ya umeme ambayo inalitafuna Taifa letu.

3.2.6 **Mheshimiwa Spika,** Kamati imejiridhisha kuwa Bodi ya Shirika la Ugavi wa Umeme Nchini (TANESCO) bila sababu zozote za msingi ilikataa mapendekezo ya Menejimenti ya Shirika ya kutoruhusu uhotwaji wa fedha kutoka Benki Kuu akaunti ya Tegeta ESCROW na hivyo kusababisha kulikosesha Shirika fedha zake inazohitaji sana kutokana na hali mbaya ya Shirika. Ikumbukwe kuwa Shirika la TANESCO lilipata hasara ya shilingi bilioni 467.7 katika mwaka wa fedha unaoishia Desemba 31, 2013. Hasara hiyo imekuwa ikiongezeka mwaka hata mwaka toka mwaka 2010 (bilioni 5), 2011 (bilioni 43), 2012 (bilioni 177) na hivyo hadi kufikia Desemba 31, 2013, jumla yote kuu ya hasara (accumulated loss) ilikuwa imefikia shilingi trilioni 1.45.

Kamati pia imethibitisha kuwa Bodi ya TANESCO mpaka sasa haijatekeleza hukumu ya ICSID 2 na kukokotoa upya viwango vya malipo ya '*capacity charges*' na hivyo kupelekea TANESCO na Serikali kuendelea kuilipa IPTL/PAP kila mwezi shilingi Bilioni 4.5

(\$2.6m kila mwezi) izalishe au isizalishe umeme. Kamati inaitaka Serikali kuvunja mara moja Bodi ya TANESCO na TAKUKURU iwafungulie mashtaka ya matumizi mabaya ya ofisi wajumbe wote waliohusika kupitisha maamuzi hayo ya kifisadi, ili iwe fundisho kwa wajumbe wengine wa bodi za Mashirika ya Umma kwamba watahukumwa kwa maamuzi mabovu wanayoyafanya.

3.2.7 **Mheshimiwa Spika**, Kamati imethibitisha kuwa Katibu Mkuu wa

Wizara ya Nishati na Madini aliingia makubaliano ya kutoa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW bila kujiridhisha kikamilifu kuwa maamuzi ya hukumu ya ICSID 2 yalikuwa bado kutolewa na hivyo kusababisha fedha kutolewa bila kukokotoa upya gharama za '*capacity charges*', jambo ambalo limesababisha kupoteza fedha za umma.

Vile vile, Kamati imebaini kuwa, Katibu Mkuu hakufanya uchunguzi wa kina (due diligence) kujiridhisha uhalali wa Kampuni ya Mechmar kuuzwa kwa Piperlink na baadaye kuuzwa kwa PAP, na hivyo kusababisha fedha za akaunti ya Tegeta ESCROW kulipwa kwa asiyestahili na kinyume cha Mkataba wa akaunti ya Escrow. Kwa maana hiyo, Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati na Madini,

pengine kwa uzembe wake ama kwa kukusudia kwa sababu anazozijua yeye mwenyewe zaidi, amesaidia uchochwaji na hatimaye utakatishaji wa fedha haramu.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imethibitisha uzembe wa hali ya juu uliofanywa na Katibu Mkuu huyo, kushindwa kujiridhisha kama masharti ya Sheria ya kodi ya Mapato Sura ya 333, Kifungu cha 90(2) yalitekelezwa. Kifungu hicho kimsingi kinaitaka mamlaka ya *'approval'* ya uhamishaji wa Makampuni kutotambua Kampuni mpaka kwanza kodi za uhamishaji ziwe zimelipwa na hati za malipo ya kodi zimetolewa na mamlaka ya kodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kuwa uteuzi wa Katibu Mkuu huyu utenguliwe, na TAKUKURU wamfikishe mahakamani mara moja, kwa kuikosesha Serikali Mapato, matumizi mabaya ya ofisi na kusaidia utakatishaji wa fedha haramu.

3.2.8 **Mheshimiwa Spika,** Kamati imethibitisha kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini alisema uongo Bungeni kwa kutamka kauli ambazo zilizokuwa na lengo la kupotosha umma kuhusu akaunti ya Tegeta ESCROW ikiwemo kutoa kauli ambazo zingeweza

kusababisha Nchi kuingia kwenye mgogoro wa kidiplomasia na nchi ya Uingereza.

Kamati inapendekeza kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini (Madini) achukuliwe hatua kali za kinidhamu ikiwemo kutenguliwa uteuzi wake. Kamati pia inapendekeza kuwa Naibu Waziri huyu afikishwe mbele ya Kamati ya Bunge ya Maadili ili aadhibiwe kama Mbunge kwa kusema uwongo Bungeni ili liwe fundisho kwa wabunge wengine kuhusiana na kauli wanazotoa ndani ya Bunge lako tukufu.

3.2.9 Mheshimiwa Spika, Kamati imethibitisha kuwa Waziri wa Nishati na Madini amekuwa, mara kwa mara, akilipotosha Bunge lako tukufu na Taifa kwa ujumla kuhusiana na Fedha za Akaunti ya Tegeta ESCROW kwamba ndani ya fedha hizo hakukuwa na fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, hata mtu wa kawaida angeweza kujua kwamba washirika wa 'Tegeta Escrow Account' ni akina nani na masharti ya kutoka kwa fedha hizo kwenye akaunti ni yapi kwa mujibu wa Mkataba wa uendeshaji wa akaunti hiyo.

Hata hivyo, katika hali ya kushangaza, aidha kwa makusudi ama kwa sababu anazozijua vizuri zaidi mwenyewe, Waziri wa Nishati ananukuliwa kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge, Kwa nguvu kubwa na kwa kujiamini, akitetea uchochwaji wa fedha hizo kinyume na masharti ya Mkataba wa Escrow.

Aidha, Kamati imebaini kuwa Waziri wa Nishati na Madini ndiye alikuwa dalali mkuu aliyewakutanisha Bwana Harbinder Singh Sethi na Bwana James Rugemalira, tena katika ofisi ya Umma; na pengine hii ndiyo iliyokuwa sababu ya upotoshaji huu. Waziri wa Nishati na Madini alifanya udalali huo akijua dhahiri kuwa Bwana Sethi hana uhalali wa kisheria kufanya biashara kwa jina la IPTL.

Iwapo Waziri wa Nishati na Madini angetimiza wajibu wake ipasavyo, Fedha za Tegeta ESCROW zisingelipwa kwa watu wasiohusika, na Nchi ingeweza kuokoa mabilioni yaliyopotea kama kodi za VAT, *Capital Gain Tax* na Ushuru wa Stempu ambazo ni sawa na takribani shilingi bilioni 30.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kuwa Mamlaka yake ya uteuzi itengue uteuzi wa Waziri wa Nishati na Madini kutokana sababu hizo zilizoelezwa.

3.2.10 **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kukua na hivi sasa kukomaa kwa vitendo haramu vya wizi wa fedha ama mali za umma na kukua ama kukomaa kwa vitendo vya rushwa kubwa na uhujumu uchumi, inapendekezwa kwamba Bunge lako Tukufu liridhie kuitaka Serikali kuanzisha kitengo maalumu cha kushughulikia rushwa kubwa (*grand corruption*) kitakachokuwa na nguvu ya kuendesha mashtaka kwa uhuru kamili, na kwamba Bunge lako Tukufu liridhie kuanzishwa kwa Mahakama Maalum ya kushughulikia Rushwa kubwa itakayoshughulikia kesi za rushwa zitakazokuwa zikipelekwa kwake na kitengo maalum cha kushughulikia rushwa kubwa.

3.2.11 **Mheshimiwa Spika,** Kamati imethibitisha kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa ushauri ulioipotosha Benki Kuu ya Tanzania kuhusiana na hukumu ya Jaji Utamwa J. Kwa kutumia madaraka yake vibaya, Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliagiza kodi ya Serikali yenye thamani ya shilingi 21 bilioni isilipwe

na hivyo kuikosesha Serikali mapato adhimu. Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kujua na kwa makusudi alilipotosha Bunge na Taifa kwamba mgogoro uliopelekea kufunguliwa kwa Akaunti ya ESCROW ulikuwa ni mgogoro wa Wanahisa wa IPTL badala ya mgogoro kati ya TANESCO na IPTL. Kamati inapendekeza kuwa uteuzi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali utenguliwe mara moja na kisha afikishwe mahakamani kwa matumizi mabaya ya Ofisi yaliyopelekea Serikali kupoteza mabilioni ya fedha.


3.2.12 **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Waziri Mkuu kuhusiana na suala hili, Kamati iliipitia kwa umakini Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 iliyoainisha Kazi na Mamlaka ya Waziri Mkuu na kubaini kuwa, kwa mujibu wa Ibara ya 52 (1):

"Waziri Mkuu atakuwa na madaraka juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano."

Na, Ibara ya 52 (2), inayosema;

“Waziri Mkuu atakuwa kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni.”

Kisha Kamati ikajiuliza maswali kadhaa. Kwa mfano katika kutaka kubaini ukweli na kujiridhisha Kamati ilijiuliza maswali yafuatayo kuhusu Waziri Mkuu:

- 
- (a) Je, Waziri Mkuu alikuwa anajua sakata la utoaji wa fedha katika Akaunti ya Tegeta ESCROW?
 - (b) Je, Waziri Mkuu alitimiza wajibu wake kwa mujibu wa Ibara ya 52(1)?
 - (c) Je, Waziri Mkuu wakati akitoa matamshi yake Bungeni alikuwa akitimiza wajibu wake kwa mujibu wa Ibara ya 52 (2)?
 - (d) Je, nini maana, uzito na ukweli wa matamshi ya mara kwa mara ya Waziri Mkuu ndani na nje ya Bunge kuhusiana na suala hili?
 - (e) Je, Waziri Mkuu alitoa maamuzi au maelekezo yoyote ya kuzuia jambo hili lisifanyike?

Mheshimiwa Spika, Baada ya kupitia vielelezo vilivyomo kwenye ripoti ya CAG, Kamati imejiridhisha pasipo mashaka kuwa, Waziri Mkuu, alikuwa ana taarifa zote kuhusiana na mchakato mzima wa kuchotwa fedha kutoka katika akaunti ya ESCROW.

Ushahidi ulioletwa na ofisi ya CAG kwenye Kamati unaonyesha kuwa Waziri Mkuu alikuwa akipata taarifa za jambo hili. Na Kamati imesikitishwa kuona kuwa Waziri Mkuu hakuchukua hatua zozote kuzuia muamala huu usifanyike.

Mheshimiwa Spika, Kamati, kwa kuzingatia kielelezo namba 22, inathibitisha bila shaka kwamba, Waziri Mkuu alikuwa analijua jambo hili vizuri na kwamba aliridhia muamala huu ufanyike. Ndiyo maana katika maelezo yake ya Bungeni mara kadhaa Waziri Mkuu alithibitisha kuwa fedha za Escrow hazikuwa fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Julius Nyerere katika kitabu chake cha Uongozi Wetu na Hatma ya Tanzania aliandika:

*“...kubadili Waziri Mkuu sio jambo la ajabu. Ndugu
Rashid Mfaume Kawawa alikuwa Waziri Mkuu wangu*

kwa muda mrefu. Hakuwa amefanya kosa lolote; lakini nilitaka kumbadili na kuteua Waziri Mkuu mwingine. Nilimwita, nikamwambia hivyo. Tukakaa pamoja mimi na yeye, tukashauriana na kukubaliana nani anafaa kushika nafasi yake. Nikamteua Hayati Edward Moringe Sokoine. Najua kuwa watu wa aina ya Rashidi Kawawa ni adimu sana Duniani, hawazaliwi kila siku; hata hivyo ni jambo la kushangaza kidogo kwamba viongozi wetu wa Mageuzi, hata bado hatujafa, wanaona kuwa ni kosa kuwakumbusha kuwa vyeo walivyonavyo ni dhamana. Wanadhani kuwa Uwaziri ni Usultani; ukishakuwa Sultani utakufa sultani! Nadhani wanakosea. Nchi hii imewahi kung'oa Masultani wa kila aina. Tukianza kuvumilia Masultani wa kuchaguliwa, tutapanda mbegu ya Masultani wa kuzaliwa. Narudia; kumbadili Waziri Mkuu sio jambo la ajabu. Anaweza kujiuzulu, anaweza kufukuzwa Nchi isitikisike. Lakini huwezi kumtimua Rais wa Nchi bila kuitikisa Nchi yenyewe. Ni vizuri jambo hili likatamkwa waziwazi na likaeleweka sawasawa. Maana watu wengine wananong'ona nong'ona kuwajibika kwa Rais kana

kwamba ni jambo la mchezo mchezo tu. Kulazimika kumchukulia hatua Rais wa nchi ni mkasa na balaa kwa Nchi yeyote ile."

Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba viongozi wenye mamlaka makubwa wanapaswa kila wakati kukumbuka kauli ya muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Muasisi wa Muungano, Sheikh Thabit Kombo, ambaye alikuwa akipenda kusema *'weka akiba ya maneno'*.

Ni wazi kwamba maneno ya Waziri Mkuu hapa Bungeni yaliuaminisha umma kuwa fedha zile siyo fedha za umma kiasi kwamba gazeti la Serikali la Daily News la tarehe 1 mwezi Mei, 2014, likachapisha habari yenye kichwa kikubwa cha habari **'IPTL clean Deal – Pinda'**. Na ofisi ya Waziri Mkuu haikukanusha.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza kuona kwamba, jambo kubwa na zito kama hili lingeweza kufanyika bila ya mamlaka za juu, hususan Mhe. Waziri Mkuu kufahamu.

Mheshimiwa Spika, kwa uzito na unyeti wa jambo hili, kwa vyovyote vile, Waziri Mkuu anapaswa kuwajibika kwa kauli zake na kwa kutokutekeleza wajibu wake wa kikatiba ipasavyo, ili kurejesha imani ya wananchi kwa serikali yao na viongozi wao wa kisiasa.

3.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru sana kwa kuiamini Kamati yetu kwa kuikabidhi jukumu hili nyeti. Nakuhakikishia kwamba kazi hii imetekelezwa kwa haki iliyojengwa katika msingi wa Taarifa ya Ukaguzi Maalum wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na vyanzo vingine muhimu vikijumuisha maelezo ya Ofisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA).

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa shukrani za dhati kwa vyombo vya habari kwa kuwapasha habari Watanzania kuhusiana na suala hili. Kwa namna ya pekee kabisa Kamati inalipongeza gazeti la *The Citizen* kwa msimamo wake thabiti bila kujali vitisho.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu inayo imani na Bunge Lako Tukufu kwamba litaitumia Taarifa hii ipasavyo katika kutekeleza Wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali itekeleze wajibu wake katika misingi ya haki, uadilifu, uzalendo, usawa, uwazi na uwajibikaji. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwani katika kipindi chote cha kuandika Taarifa hii mlitulia moyo kwa kuonesha dhahiri kwamba mnaihitaji Taarifa yetu ijadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuishukuru Ofisi ya Spika kwa maelekezo thabiti ya namna ya kutekeleza jukumu hili.

Naomba pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashillilah na Wajumbe wa Sekretarieti yake kwa ushauri makini katika kipindi chote ambacho Kamati ilikuwa ikitekeleza jukumu hili. Kipekee nawashukuru pia Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ndg. Francis Mwakapalila, Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Dkt. Edward Hoseah na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato nchini, Bw. Rished Bade kwa ushirikiano walioipatia Kamati.

Mwisho, nawashukuru Watumishi wote wa Bunge na vyombo vingine vya kiusalama vilivyohusika katika kuisaidia Kamati kutekeleza jukumu lake.

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako tukufu lipokee Taarifa hii, lijadili na kupitisha mapendekezo yote tuliyoyatoa kuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.



Zitto Zuberi Kabwe, Mb.

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC)

26 NOVEMBA, 2014